Nipashe
Alhamisi Novemba 9, 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581489
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**MAHAKAMA** yapokea nyaraka matengenezo gari mke bilionea Msuya

UKURASA 4



**MWALIMU** aliyejeruhiwa mapanga ahofia maisha yake

UKURASA 5



UKURASA 19

**ISRAEL** yasitisha mapigano kupisha misaada ya kijamii

# Adha usafiri treni Dar yamwibua RC

**BAADA** ya kushukiwa na Rais, ainyoshea kidole TRC, wananchi waeleza taabu, kero wanazopata...

*Endelea Ukurasa wa 2*



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (kulia), akisikiliza kero za abiria wa treni ya 'Mwakyembe', eneo la Gerezani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbaroni madai ya kutengeneza biskuti zilizochanganywa bangi



UKURASA 3

UKURASA WA 23

## YANGA YAPANGA KUSHUSHA 'MASHINE' MPYA DESEMBA

KATIKA kuhakikisha wanatimiza malengo yao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa, uongozi wa Yanga umesema utaboresha kikosi chao wakati wa dirisha...




Rais Samia Suluhu Hassan akishiriki mijadala kuhusu fursa mbalimbali za uwekezaji Afrika wakati wa mkutano wa Jukwaa la Uwekezaji Afrika jijini Marrakesh, Morocco jana. Wengine ni Rais wa Comoro, Azali Assoumani (wa pili kushoto), Rais wa Sierra Leone, Julius Maada (kushoto) na Waziri Mkuu wa Rwanda, Dk. Edouard Ngirente. **PICHA: IKULU**

## Simulizi maisha mjane aliyefungwa miaka 22 kukutwa na nyama ya swala

UKURASA 3

**MICHEZO** **WAZIRI AITAKA SIMBA KWENDA TAKUKURU** UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (kulia), akikabidhi zawadi ya picha ya Mlima Kilimanjaro kwa Balozi wa Australia nchini mwenye makazi yake jijini Nairobi, Kenya, Luke Williams, aliyefika katika Ofisi Ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam jana, kuaga baada ya kumaliza muda wake wa uwakilishi. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Adha usafiri treni Dar yamwibua RC

**Na Peter Orwa**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amefanya ziara ghafla kupata uhalisia wa adha ya usafiri wa treni jijini Dar es Salaam huku akibainisha kuwa ni agizo la Rais Samia Suluhu Hassan.

Ziara hiyo ya Chalamila na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, imefanyika siku moja baada ya gazeti hili kuchapisha habari kuhusu hali mbaya ya usafiri wa daladala treni za Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Habari hiyo ilionyesha abiria walivyojaa, kuning'inia kwenye kichwa cha treni, wengine wakiwa nje kwenye milango iliyofungwa na sehemu ya nyuma kwenye maungio ya treni.

Nipashe iliyokuwa ikifuatilia hali inayojiri katika usafiri huo kwa siku kadhaa, ilishuhudia safari ya mwisho treni hiyo Jumatatu wiki hii, ikiondoka Gerezani saa 3.35 usiku badala ya saa 2.15 ikiwa imejaa sana licha ya kuongezwa behewa tatu.

Ilirejea mjini kutoka Pugu saa 5.00 usiku badala ya saa 3.15 kama ratiba inavyotaka. Juzi iliondoka saa 2.30 lakini ikiwa imejaa sana na kukaripotiwa baadhi ya abiria kuachwa kwa kukosa nafasi.

Katika ziara hiyo jana asubuhi, Chalamila aliambatana na Katibu Tawala wa Mkoa, Rehema Madenge na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo. Katika safari hiyo, Chalamila akitaka kubaini kasoro ambazo alisema baadhi alishaanza kuzifanyia kazi.

Viongozi hao walisafiri kwa treni hiyo iliyoanza safari saa 1. 15 asubuhi stesheni ya Gerezani hadi Pugu na kufika saa 2:00 kisha kurejea mjini ilikofika saa 3:15. Katika safari hiyo, viongozi hao walipokea pia maoni na kero kutoka kwa wananchi.

Wengine waliokuwapo katika safari hiyo ni Menejimenti ya TRC iliyoongozwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Amina Lumuli, Mkurugenzi wa Uendeshaji, Focus Makoye na Kamanda wa Polisi Reli, Sebastian Mbuta. Pia walikuwamo uongozi wa Wakala wa Barabara (TANROADS) na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

Chalamila jana baada ya kushuhudia na kupata maoni ya abiria, pia aliorodhesha kasoro za utendaji, akisema inaanzia na uendeshaji usioridhisha wa TRC. Alisema abiria wanaongezeka kutokana na hali mbaya ya Barabara ya Nyerere, hasa kutokana na ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi unaoendelea ambao umesababisha barabara kutopitika, hasa baada ya mvua kubwa iliyonyesha siku kadhaa hivi karibuni.

Chalamila alitumia vipaza sauti ndani ya treni akifafanua aliyobaini na kukaribisha maoni, huku akimbebesha jukumu kila anayehusika kufafanua malalamiko ya abiria, akiorodhesha zaidi ya madai 10 yaliyomfikia.

**HALI YA MALALAMIKO**

Chalamila, wakati treni ikiendelea na safari, aliyataja malalamiko yanayojumuisha treni kutozingatia ratiba; kukosekana sehemu za kujisitiri stesheni hasa wakati wa mvua na mabehewa kukosa vyoo.

Mengine ni kwa wanafunzi kuwa na mabehewa ambayo hayatoshi na yanavamiwa na watu wazima na kutokuwamo vyumba vya kuhifadhi wenye hali ngumu kama wajawazito na wenye ulemavu.

Kasoro zingine ni idadi chache za safari za treni kila siku ambazo ni mara tatu kwenda na kurudi asubuhi hadi saa 5:00 usiku, pia mara tatu hadi saa 3.45 usiku na kutokuwapo kwa safari siku za Jumamosi.

Pia ilibainika kuwa mabehewa yaliyopo hali si rafiki, hayana feni, watumishi wakata tiketi 'TT' kuuza tiketi mbili, abiria kutorejeshewa fedha wanapoachwa, treni kuondoka imejaa na hakuna nafasi na watu kupishana mlangoni.

Katika kutoa ufafanuzi, Makoye alitumia mfano wa juzi kwamba walirejeshewa pesa, nauli ya Sh. 600 lakini ghafla abiria waliokuwa wanafuatilia hoja, wakalipuka na kusema 'uongoo'' hali iliyosababisha kurekebisha kauli na kusema: "Ni abiria watatu tu ndio wamerejeshewa."

Lumuli, katika ufafanuzi wake, alisema sehemu kubwa ya malalamiko yako nje ya uamuzi wa papo kwa hapo na menejimenti inayabeba kama changamoto kwenda kuyafanya kazi.

Aliyataja mambo ambayo wana uwezo nayo kuwa ni kuongeza idadi ya safari na kukabili ubadhirifu kwenye tiketi. Kuhusu safari za Jumamosi, aliahidi kufanyia kazi kwa kuwa ni siku ambazo treni inafanyiwa matengenezo.

Baada ya treni kufika Gerezani saa 3.20, Chalamila ambaye alionyesha anafahamu mengi yanayojiri TRC, alitumia ngazi ya behewa alilokuwamo kama jukwaa kupokea kero.

Hapo ndipo umma wa abiria ulipolipuka tena, kumlalamikia mmoja wa askari polisi anayetumika mahali hapo kwamba anawanyanyasa na kutumia fimbo ndefu kuwachapa na kuwatukana wanaponunua tiketi.

"Huyoo hapoooo (polisi)..." Ni kelele za abiria waliomnyoshea kidole askari huyo aliyekuwa jirani na Chalamila akamwamuru apande kwenye behewa alilokuwamo yeye na Kamanda wa Polisi Reli, akimkabidhi kwa hatua zaidi.

Muda mfupi baadaye, Chalamila alijumuika na uongozi kando ya reli akimwagiza Kamanda Mbuta kuchunguza tuhuma hizo na kuchukua hatua, huku akiahidi naye ataendelea kuchunguza mambo yaliyojiri kwa njia anazozijua.

"Ninyi (uongozi wa TRC) nendeni mkakae kikao mtafute majibu sasa hivi," alisema Chalamila na kuongeza kuwa: "Nami niko nanyi wiki mbili hizi kujua kwa njia ninazozijua.

"Ni afadhali muue safari nyingine (ya Ubungo) kuliko hivi. TRC ni shirika kubwa hamna hata kinanda cha kupumzika. Hawa abiria si wajinga, wana akili na wanaona sana."

Chalamila pia aliiagiza TANROADS kukaa na mkandarasi anayojenga njia ya mwendokasi kuandaa njia za kando kurahisisha magari kupita ili kupunguza adha ya abiria.

Usafiri wa treni daladala, maarufu kama 'Treni ya Mwakyembe, ulianzishwa mwaka 2013 na aliyekuwa Waziri wa Uchukuzi, Dk. Harrison Mwakyembe, kwa treni kufanya safari kati ya Pugu na Stesheni Kuu, lakini baadaye ikabadilishwa kuishia Gerezani kutokana na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Treni hizo zina wastani wa mabehewa 16 na kila moja ikijaa, inachukua abiria kati ya 250 na 300. Lakini sasa kutokana na hali iliyopo kuanzia wiki hii, kuna wastani wa mabehewa hadi 20 kwa safari moja.

Pia kuna safari za Gerezani hadi Ubungo na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ambayo ina huduma kama hizo kati ya stesheni kuu Buguruni na Pugu Mwakanga.

## Samia ataja afya, elimu vipaumbele vyake kukuza uchumi

**Na Restuta James**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema afya na elimu ni sekta zake za kipaumbele kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi na maendeleo ya nchi.

Aidha, amesema mpango wa 'Building Better Tomorrow (BBT), unalenga kuongeza mchango wa sekta ya kilimo kwenye pato la taifa kutoka asilimia nne za sasa hadi 10 mwaka 2030.

Rais Samia aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa Jukwaa la Uwekezaji Afrika, unaofanyika nchini Morocco.

"Nimeamua kuchukua baadhi ya mambo kama ajenda zangu binafsi mojawapo ni sekta za elimu na afya kwa kutambua nafasi yake kwenye kukuza uchumi kwenye afya nimeamua kuimarisha ubora wa huduma," alisema.

Alisema ili kufanikisha hilo, serikali inaweka nguvu katika ujenzi wa vituo vya afya, kuongeza dawa na vifaa pamoja na watumishi wa afya kwenye zahanati na hospitali za umma.

Alisema kinachofuata sasa ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya kwa usawa na ndio maana serikali imetunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote.

"Kadhalika masuala ya lishe na uzazi ni mambo serikali inayapa kipaumbele kwa ajili ya ubora wa watoto wa Tanzania," alisema Rais Samia.

Vile vile, alisema kwenye elimu, serikali imeamua kutoa elimu bila malipo pamoja na kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokosa nafasi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya ujauzito.

"Kubwa zaidi ni kwamba ili tuwe na maendeleo endelevu tumeamua kuwashirikisha wanawake na vijana kwenye kilimo kupitia programu ya BBT nia ni kuingiza kundi hili kubwa kwenye shughuli za kilimo," alisema.

Alisema lengo la serikali yake ni kuona sekta ya kilimo cha mazao, ufugaji, uvuvi na urinaji wa asali zinakua za kisasa na kibiashara ili ziweze kuzalisha ajira na malighafi za kutosha.

"Hii inajumuisha uwekezaji mkubwa wa pembejeo, mifumo ya umwagiliaji na majukwaa ya kidijitali ambayo yanatoa fursa kwa vijana kupata taarifa za masoko na pembejeo," alisema.

Rais Samia aliishukuru Benki ya Maendeleo Afrika (AFDB), kwa kusaidia serikali katika utekelezaji wa BBT na kwamba matarajio ni kuwa hadi mwaka 2030, sekta ya kilimo itachangia pato la taifa kwa asilimia 10 kutoka nne ya sasa.

# Simulizi maisha mjane aliyefungwa miaka 22 kukutwa na nyama ya swala

**Na Francis Godwin**, IRINGA

MAPYA yameibuka kuhusu maisha na familia ya Maria Ngoda, mjane aliyefungwa jela miaka 22 kwa kosa la kukutwa na vipande 12 vya nyama ya swala kinyume cha sheria.

Dada wa mjane huyo, Abelia Myumbilwa, akizungumza na mwandishi wa habari hii, nyumbani kwake, Mtaa wa Zizi, Kata ya Isakalilo, Manispaa ya Iringa jana, alisema Maria alikuwa akiishi kwa kazi za kutumwa na wakazi wa eneo hilo ikiwamo kutembeza samaki kwenye vilabu vya pombe za kienyeji na kulipwa ujira kati ya Sh. 1,000 na 2,000 kwa siku .

"Sisi kama familia tumepigwa na butwaa baada ya kusikia ndugu yetu amehukumiwa kifungo cha miaka 22 jela. Hadi sasa, hatujui nini cha kufanya kwani hata kama gharama ya kuweka wakili itakuwa Sh. 50,000 hakuna mwenye uwezo," alisema huku akitokwa machozi.

Alisema kabla ya hukumu hiyo, Ngoda alikuwa mahabusu kwa miezi minne kutokana na ndugu zake ambao walikuwa wamemdhamini kujitoa kwa kuchoshwa na usumbufu wa kwenda kuripoti polisi kila siku. Muda wote alikuwa mahabusu na hata siku ya hukumu alitokea huko.

Alisema, Ngoda ana watoto wanne wakiwamo wakubwa watatu na mmoja ni mdogo ambaye alishindwa kuendelea na elimu ya sekondari na akiwa kidato cha pili kwa kushindwa kulipa michango mbalimbali ya shule.

"Mchango ambao ulikuwa mkubwa, alitakiwa mama yeke kumlipia na hakuna aliyekuwa na pesa ya kulipa, ulikuwa Sh. 20,000 na huo ndio uliosababisha mtoto kuacha shule hadi sasa," alisema.

Kutokana na hali yake, aliulizwa kama alifikiwa na mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na kujibu kuwa hakufikiwa licha ya kuwa na sifa.

**OMBI KWA SERIKALI**

Myumbilwa aliiomba serikali kumsaidia mjane huyo na familia yake ambayo ilikuwa ikitegemea kuishi kwa pesa zinazotafutwa na mama huyo.

Alisema mbali na kutegemea kazi za vibarua, vikiwamo vya kufua nguo, kulima na kuuza samaki au kutembeza mboga za watu mitaani, pia alikuwa akijihusisha na kuponda mawe milimani ili kujikimu.

Janeth Mdindile, mtoto mdogo wa Ngoda, alisema hawajui hatima ya mama yao, hawajui hata sehemu ya kuanzia kukata rufani. Alibainisha kwamba wakati akiwa mahabusu, kuna watu walionyesha kumsaidia lakini walighairi baadaye.

Majirani wanaomzunguka Ngoda walisema katika maisha yake, hawajawahi kumwona akiuza nyama zaidi ya samaki na mboga za majani na hata siku waliposikia amekamatwa walijiuliza amepata wapi.

Sarah Kalinga, mmoja wa majirani hao, alisema hawana uhakika kama kweli ilikuwa nyama ya swala. Alisema licha ya mpango wa kukata rufani, ni vyema nyama hiyo ikapimwa kujua kama kweli ni swala. Pia alisema ni vyema pia anayedaiwa kumpatia nyama hiyo ajulikane yuko wapi na kwa nini vyombo vya dola havikumtafuta mhusika.

Wakati akijitetea bila usaidizi wa wakili, mjane huyo alikiri kuwa alikutwa na ndoo yenye nyama hiyo ambayo alidai alikabidhiwa na mtu aliyemtambua kwa jina la Fute bila kujua ina nyama ya nini.

Alidai kuwa alilazimishwa abebe ndoo hiyo na kufikishwa kituoni kisha kufunguliwa kesi ya kukutwa na nyara za serikali sambamba na kosa la uhujumu uchumi.

Diwani wa Isakalilo, Deo Msemwa, akizungumzia hatua ya mahakamaa, alisema wameshangazwa na hukumu hiyo.

Kuhusu Ngoda kutokuwapo kwenye mpango wa TASAF, alisema hajui kwa nini kwa kuwa alikuwa na sifa zote. Pia alisema anafuatilia tukio la mtoto wake kushindwa kuendelea na masomo kwa kukosa michango.

Wakili wa Kujitegemea, Emmanuel Chengula, alisema kumekuwapo na hoja nzito kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari juu ya hukumu hiyo japo wengi walielekeza lawama kwa hakimu na mahakama kuwa si sawa kwa mujibu wa adhabu aliyopewa.

**KAULI YA TLS**

Mwenyekiti wa TLS Iringa, Wakili Moses Ambindwile, alisema wameanza mchakato wa kumsaidia kisheria mjane huyo na tayari wameshapata nakala ya hukumu ambayo wanaipitia kabla ya kukata rufani ndani ya siku 10 za kisheria.

Hukumu hiyo ilitolewa Novemba 3, mwaka huu na Hakimu Mkazi Mkuu, Said Mkasiwa, baada ya kujiridhisha kuwa ni kweli mjane huyo mwenye watoto wanne, alikutwa na ndoo iliyokuwa na nyama hiyo yenye thamani ya Sh. 900,000 kinyume na sheria .

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Mkasiwa alisema kosa hilo ni kinyume cha kifungu cha 86 (1) (2) (c) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho na kifungu cha 59 (a) (b) cha mabadiliko ya sheria ya mwaka 2016.



Mwandishi wa habari wa gazeti hili, Mkoa wa Iringa, Francis Godwin (kulia), akifanya mahojiano na familia ya mjane Maria Ngoda aliyefungwa jela miaka 22 na Mahakama ya Hakimu Mkazi Iringa kwa kosa la kukutwa na vipande 12 vya nyama ya swala. **PICHA: SELEMAN YUSUPH**

# Mbaroni madai ya kutengeneza biskuti zilizochanganywa bangi

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania (DCEA) imewakamata watu 16 mkoani Dar es Salaam, wakituhumiwa kutengeneza biskuti kwa kuchanganya na bangi iliyosindikwa, maarufu kama Skanka.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Aretas Lyimo, alisema jana kuwa katika tukio hilo, pia wamegundua kiwanda bubu cha kusaga bangi (Skanka) eneo la Kawe na kwamba watuhumiwa hao walikuwa wakiendelea na uzalishaji wa biskuti hizo.

Aidha, mamlaka hiyo imetoa angalizo kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo kuwa makini na bidhaa za biskuti, juisi, keki, jamu na tomato sauce pamoja na matumizi ya shisha kwa kuwa watu wasio waaminifu wanatengeneza kwa kuchanganya na bangi hiyo.

"Watu hao tuliowakamata walikuwa wanajihusisha na utengenezaji wa bidhaa hizo. Tumewakamata maeneo ya Kawe wakiwa na mtambo wa kusaga skanka na vifaa vya kutengeneza biskuti za bangi, wote wanashikiliwa," alisema.

Lyimo pia alisema watu hao 16 waliokamatwa sita kati yao tayari wamefikishwa mahakamani na watu 10 waliobakia watafikishwa baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Alisema vijana na watoto wanapaswa kuwa makini na ulaji wa bidhaa hizo zilizotajwa kwa kuwa watu wasio waaminifu wanachanganya na bangi ili kurahisisha uuzwaji wake na kusambazwa kwa urahisi zaidi.

Alisema, Skanka imekuwa ikiingizwa nchini kutoka nchi za jirani baada ya kuadimika nchini bangi za kawaida kutokana na operesheni wanayoendelea kuifanya ya kuteketeza mashamba ya bangi katika mikoa ya Mara, Morogoro, Arusha na Iringa.

Katika operesheni waliyoiendesha hivi karibuni kwenye mipaka na fukwe za Bahari ya Hindi, alisema pia wamekamata bangi ya skanka kilogramu 423.54.

"Katika mzigo huu, kilogramu 158.54 zimekamatwa eneo la Kigamboni hapa Dar es Salaam zikiwa zimehifadhiwa ndani ya mabegi ya nguo tayari kusafirishwa, kilogramu 265 zilikamatwa katika matukio tofauti katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini zikiwa zimefichwa ndani ya magari kwa kuchanganywa na bidhaa nyingine yakiwamo makasha yenye matunda aina ya 'Apple'," alisema Kamishna Jenerali Lyimo.

**SHISHA**

Katika hatua nyingine, Kamishna Jenerali Lyimo alisema kwa sasa mamlaka hiyo ipo kwenye utaratibu wa kuandaa sheria ya matumizi ya shisha ili kuondoa matumizi ya bangi kwenye bidhaa hiyo.

Alisema kwa sasa watu wasiowaaminifu wanatumia dawa hizo za kulevya kwenye shisha na kupelekea vijana wengi kuathirika.

"Kwa sasa siwezi kuliongelea sana kwa sababu liko kwenye taratibu za kukamilisha sheria ya kupambana na shisha. Pale litakapokuwa limekamilika basi litawekwa wazi lakini ni kweli kwa sasa vijana wengi wanaathirika na shisha inayochanganywa na bangi," alisema.

Akizungumzia baadhi ya waraibu wa dawa za kulevya kutumia dawa tiba zenye kilevi kama sehemu ya kujipoza na 'arosto' ya dawa hizo, Lyimo alikiri kuwapo kwa matumizi hayo na tayari wameshaanza mchakato wa kukutana na watengenezaji, waingizaji na wasambazaji wa dawa hizo zinazotumika hospitalini kuangalia namna ya kudhibiti matumizi yake.

"Watu hawa wanaotumia madawa tiba ambayo yanaruhusiswa hospitalini wanafanya hivyo kutokana na kuadimika kwa madawa ya kulevya kama Cocain, Herroin ambayo kwa kiasi kikubwa tumedhibiti uingizwaji wake hapa nchini na usambazwaji.

"Ziko dawa yanayoruhusiwa hospitalini kwa ajili ya kuwatibu watu wenye matatizo hasa wale wenye maumivu makali, watumiaji hawa wa dawa za kulevya wakipata hizi dawa tiba wanatumia kama mbadala wa dawa za kulevya, hili tunalifanyia kazi kuangalia namna ya kudhibiti matumizi yasiyofaa ya dawa tiba hizi," alisema.

Kamishna Lyimo aliwaomba wananchi kuendelea kushirikiana na mamlaka hiyo katika kutoa taarifa ya watu wanajihusisha na uingizaji na usambazaji wa madawa ya kuevya kwa kupiga namba ya simu ya bure ya 119.



Mkazi wa Dar es Salaam, akiwa amebeba samaki aina ya jodari baada ya kumnunua katika Soko la Kimataifa la Samaki Magogoni 'feri', jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mahakama yapokea nyaraka kuhusu matengenezo gari mke Bilionea Msuya

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imepokea nyaraka iliyozalishwa kutoka kwenye mfumo wa Kampuni ya kuuza magari ya CMC Automotors na majibu ya kampuni hiyo kwenda kwa Mkurugenzi wa Mashitaka nchini (DPP) kama kielelezo katika kesi ya mauaji ya Aneth Msuya, dada wa marehemu Erasto Msuya, maaruufu kama Bilionea Msuya.

Washitakiwa katika kesi hiyo namba 103 ya mwaka 2018 ni aliyekuwa mke wa Bilionea Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wote wakazi wa Arusha.

Mahakama hiyo ilifikia hatua hiyo jana, baada ya upande wa mashtaka kupitia shahidi namba nne wa utetezi, Meneja Utawala na Matengenezo wa kampuni hiyo, Ernest Msuya (65), kuiomba mahakama ipokee barua na viambatanisho kama kielelezo ambacho upande wa utetezi uliipinga.

Katika uamuzi huo, Jaji Edwin Kakolaki anayesikiliza kesi hiyo, alisema pingamizi lilitokana na viambatanisho, shahidi hakuwezeshwa kuvielezea uhusika wake kabla ya kutolewa na kukiri kwamba hoja ya Wakili Peter Kibatala kwamba shahidi hakuelekezwa ni sahihi.

"Katika viambatanisho hivi ni kweli kuna baadhi ya nyaraka mbili ni nakala, kwa hiyo haviwezi kuwa sehemu ya hiyo barua husika kwa sababu ziliambatanishwa kinyume. "Pingamizi la Kibatala sehemu linakubalika kwa kutokupokea nakala, lakini kuhusiana na vielelezo viwili, vinaweza kupokewa kama ushahidi," alisema Jaji.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, aliomba mahakama kupokea nyaraka hizo kama kielelezo baada ya shahidi kutambua barua ambayo imetoka katika ofisi yao iliyotiwa saini na mmiliki wa kampuni hiyo, Atony Haji.

"Mheshimiwa Jaji tunapinga kabisa kwa sababu hatujamsikia shahidi akisema kuna viambatanisho vyovyote. Lakini kwa upande wa barua, hatuna pingamizi kabisa kwa sababu utaratibu umefuatwa. Hivyo vingine tunapinga," alidai Kibatala.

Baada ya mahakama kupokea nyaraka ilizozalishwa kutoka kwenye mfumo kuhusiana na gari namba T 307 CDH aina ya Ford Ranger na barua ya majibu kutoka kwa mmiliki wa Haji kwenda kwa DPP, Kimweri alimwomba Jaji shahidi asome ili kuonyesha viambatanisho vilivyokuwapo.

Shahidi alisoma kwamba ni nyaraka ya kadi ya CMC Automotors ya gari namba T 307 CDH aina ya Ford Ranger ambayo lililo tengenezwa Desemba 31, 1967.

Aliendelea kudai kuwa, Mei 9,2016 gari hilo liliingia CMC saa 2:00 asubuhi na lilitoka siku hiyo hiyo saa 11 jioni na ni mali ya Kampuni ya SG Adviture Arusha.

Katika historia ya gari lilianza kutengenezwa CMC mwaka 2015 na baadaye Juni 21, 2015, Oktoba 6, 2015 na Novemba 27,2015 lilikwenda kutengenezwa kiyoyonzi. Bada ya hapo aliendelea kumhoji kama ifuatavyo;-

**Kimweri:** Sasa shahidi kwa kielelezo hiki, kabla sijaendelea mbele utakubaliana na mimi ni lini gari lilikwenda huko CMC kwa ajili ya matengenezo (akimaanisha tarehe alizozitaja)?

**Shahidi:** Sikubaliani na wewe.

Kimweri: Shahidi ni vilevile tu kwamba siku hiyo gari lilikuwa linashughulikiwa CMC Motors.

**Shahidi:** Ni kweli.

Jaji: Ni nyaraka gani uliyokuwa unasoma.

**Shahidi:** Rekodi ya matengenezo.

**Kimweri:** Kwa rekodi hiyo ya matengenezo ieleze mahakama ni tarehe ngapi, mwezi gani na mwaka gani hilo linaonekana kufanyiwa matengenezo ni kweli kuna tarehe 9/5/2016?

**Shahidi:** Sahihi kabisa gari lilikuja kufanyiwa matengenezo.

**Kimweri:** Baada ya gari hilo kushughulikiwa Mei 9,2016, pamepita muda gani kurudi tena kufanyiwa matengenezo CMC?

**Shahidi:** 19/10/2016.

**Kimweri:** Kwa rekodi hizi tangu Mei 9, 2016 hadi Oktoba 19,2016 haionyeshi kwamba gari haijawahi kufanyiwa matengenezo tena?

**Shahidi:** Ni kweli.

**Kimweri:** Na hiyo gari ni namba ngapi vile?

**Shahidi:** Ni T 307 CDH aina ya Ford Ranger.

**Kimweri:** Hebu shika kielelezo chenu DE11 ambacho kimejazwa kwa mkono. Nataka uangalie tarehe 9/5/2016 ni kweli gari hilo lilikuwa CMC?

**Shahidi:** Ni sawa tarehe hiyo.

**Kimweri:** Iambie mahakama kwa hicho kielelezo chako cha kuandika kwa mkono ukiacha tarehe 9/5/2016 ni tarehe ngapi kinaonesha gari liliingia tena CMC?

**Shahidi:** 10/8/2016.

**Kimweri:** Tutakubaliana hizo ni tarehe za kuingia gari CMC?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Kimweri:** Kielelezo ulichokitoa mahakamani vinasigana na nyaraka zilizozalishwa kutoka kwenye mfumo wa CMC kuhusiana na gari hilo.

**Shahidi:** Havisigani.

**Kimweri:** Sasa kama hakuna tofauti, ieleze mahakama tarehe iliyofuata ya gari hilo kutengenezwa kwenye gereji ya CMC.

**Shahidi:** Agosti 10, 2016.

**Kimweri:** Kwa mujibu wa kielelezo DE 11 na PE 18 iambie mahakama kama hizo tarehe kwenye nyaraka zote mbili zinalingana.

**Shahidi:** Havilingani.

Kimweri: Katika kielelezo ulichokileta mahakamani hakuna tarehe nyingine ambayo gari liliingia yaani ile ya mwisho ambayo imefungwa kabisa hapo chini kwenye kielelezo chako DE 11?

**Shahidi:** Tarehe ya mwisho kabisa ni 10/8/2016.

Kimweri: Haionekani tena ni tarehe gani ilifanyiwa 'service' tena CMC.

**Shahidi:** Hii nyaraka kazi yake ni kuingia gari na kutoka.

**Kimweri:** Baada ya kusoma kichwa cha habari cha hiyo nyaraka yako, utakubaliana na mimi kwamba ni kwa ajili ya 'services'?

**Shahidi:** Hapana si unaona kuna kilomita.

**Kimweri:** Wakili wako alikuelekeza kwenye tarehe 14/5/2046 na 15/5/2016 gari hilo lilikuwa CMC kwenye matengenezo.

**Shahidi:** Hapa kwenye nyaraka haionyeshi kama ilifanyiwa matengenezo

**Kimweri:** Wewe umesema unafanya kazi makao makuu ya CMC Dar es Salaam. Unamfahamu Mohamed Abass Mohamed?

**Shahidi:** Namfahamu.

**Kimweri:** Unamfahamu kama nani?

**Shahidi:** Meneja Uendeshaji.

**Kimweri:** Attony Haji unamfahamu.

**Shahidi:** Namfahamu.

**Kimweri:** Kama nani?

**Shahidi:** Mwenye kampuni.

**Kimweri:** Ulisema taarifa zote zipo kwenye mfumo na pia mfumo unatunza kumbukumbu sahihi hata kama zimetoka kwenye matawi mengine?

**Shahidi:** Sahihi.

**Kimweri:** Mheshimiwa Jaji naomba kumwonyesha nyaraka hii shahidi atueleze kama anaijua.

**Shahidi:** Ni barua kutoka CMC Automotors.

**Kimweri:** Nani amesaini hiyo barua?

**Shahidi:** Attony Haji.

**Kimweri:** Tukumbushe tena ni nani huyo?

**Shahidi:** Ni mwenye kampuni.

**Kimweri:** Kwenye hiyo barua kwenye anuani ni nani?

**Shahidi:** Ni Haji anamwandikia Mkurugenzi wa Mashitaka nchini (DPP).

**Kimweri:** Ukiacha sahihi ya bosi wako nini kingine umekijua?

**Shahidi:** Kuna Muhuri.

**Kimweri:** Kwa kuwa umetambua barua iliyoandikwa na bosi wako, una tatizo kama ikitolewa mahakamani kama kielelezo?

**Shahidi:** Sina tatizo.

**Kimweri:** Tunaomba ipokewe kama kielelezo pamoja na viambatanisho vyake kwa sababu shahidi hana pingamizi.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi leo kwa ajili ya kuendelea na ushahidi wa upande wa utetezi.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake, Aneth, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni, Dar es Salaam, alikiri kuhusika na mauaji hayo, katika maelezo yake ya onyo.

## Makamu wa Rais ataka wanaume kupinga ukatili

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais mstaafu wa Afrika Kusini, Dk. Phumzile Mlambo Ngcuka, amesema ni muhimu wanaume wakajumuishwa katika harakati za kimapinduzi ili kufikia usawa wa kujinsia jumuishi.

Akifungua Tamasha la 15 Jinsia na miaka 30 ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na TAPO la ukombozi wa wanawake lililowaleta pamoja wanaharakati zaidi ya 2,000 kutoka nchi 14 duniani, alisema ni muhimu wanaume wakashiriki kupigania usawa wa ajira na mishahara kwa wanawake na wanaume, kubomoa mifumo dume, kupinga ndoa za ututoni na ukatili wa kijinsia.

Dk. Phumzile ambaye aliwahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la UN Women, alisema harakati zilizofanywa na TGNP zimewezesha wengi kupata haki zao na kuwezesha usawa wa kijinsia.

"Katika harakati hizi za kimapinduzi ni muhimu sana wanaume wasiachwe nyuma, itapendekeza ikifika mahali wanaume wakisema tunataka tulipwe mshahara sawa na wanawake, kama mwanamke analipwa mshahara mdogo ifikie mahali waache kazi, kwa kufanya hivi tutafikia usawa kiuchumi," alisema.

Aidha, aliipongeza Tanzania kwa kutekeleza maazimio ya mkutano wa nne wa wanawake duniani uliofanyika Beijing China mwaka 1995 ikiwa ni miaka 28 iliyopita ambao ulileta mabadiliko makubwa duniani, na kwamba kutokana na nchi kufanya vizuri ustawi wa kijinsia umeongezeka.

"Nimefanya kazi ngazi ya kimataifa ninaweza kuona mchango wa TGNP katika kujenga uwezo kwa wanawake wa Tanzania kufanya uchambuzi wa masuala ya kijinsia. Nchi ya Colombia na Tanzania pekee wanawake wanajengewa uwezo wa kuchanganua mambo," alibainisha.

Aidha, alisema mkutano huo uliipa Tanzania heshima kubwa hasa ikizingatiwa uliongozwa na Mtanzania, Balozi Getrude Mongela, ambaye aliweka historia isiyosahaulika kwa kuwa maazimio yalisababisha mageuzi ya kisera, kimfumo na kisheria kwenye mataifa mbalimbali duniani hasa Afrika.

Mkurugenzi Mkazi wa UNWomen Tanzania, Hodan Addou akitoa salaam, alisema bado kuna matukio ya ukatili wa kijinsia ambao unahitaji nguvu ya pamoja baina ya wadau wote wa harakati za ukombozi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, zisipofanyika jitihada zaidi na kujipanga, kushikamana na kuwahusisha wanawake na wanaume itachukua miaka 300 kufikia usawa wa kijinsia, na kuzuia mabaya yote wanayotendewa watoto wa kike na kiume.

Mwenyekiti wa Bodi ya TGNP, Gemma Akilimali, alisema anajivunia kwa shirika hilo kuanzisha na kulea

mitandao mbalimbali ya uchechemuzi wa sera, mipango na bajeti zenye mrengo wa jinsia.

"Mifano michache ya mitandao hiyo ni FemAct ambao kwa sasa haupo, Mitandao ya Jinsia Ngazi ya Wilaya (Intermediary Gender Networks IGNS), Mtandao wa Vituo vya Taarifa na Maarifa ambavyo vipo katika wilaya 52 kata 72 na vimeweza kufikia watu milioni moja moja kwa moja, Mtandao wa Wanawake na Maji (Women for Water).

"Mtandao wa Bajeti Yenye Mrengo wa Jinsia (GRB alliance), Mtandao wa Wanawake Herstoria Yetu Fahari Yetu, Mtandao wa SADC Gender Alliance Tanzania (Kufuatilia utekelezaji wa Mkataba wa Jinsia na Maendeleo wa SADC) nitataja tu hii michache."

# Mwalimu aliyejeruhiwa mapanga ahofia maisha yake

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Shule ya Sekondari Makojo, Emmanuel Daghau (pichani), aliyejeruhiwa kwa mapanga, ametoka hospitalini, huku akihofia maisha yake iwapo atarudi kufundisha katika shule hiyo na kuomba serikali kumhamisha.

Daghau alikatwa mapanga Novemba mosi, mwaka huu na Jaguji Musimo katika Kijiji cha Makojo Musoma Vijijini wakati akitekeleza majukumu yake ya kazi.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, mkuu huyo wa shule, alisema alilazwa katika Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, mjini Musoma kwa muda wa siku tatu.

Alisema baada ya kutoka hospitalini anaishi mjini Musoma na familia yake akiendelea kuuguza majeraha ya mapanga yaliyotaka kumtoa uhai.

Akisimulia alivyokatwa mapanga, alisema mtuhumiwa Musimo alimfuata muda wa saa nane mchana akiwa amebebwa kwenye bodaboda na kuanza kumhoji maswali na kushambuliwa.

"Huyo jamaa tunafahamiana vizuri tu na sikujua kama yuko hivyo, ndiyo maana aliniuliza kwamba 'nilishakuja kwako kuomba amboni ya chakula' nikamjibu asubiri nimalize kuongea na simu ya kazi ndipo nimsikilize, lakini ghafla akaanza kunikata mapanga," alisema Daghau.

Alifafanua kuwa mtuhumiwa alimkata mapanga mawili kichwani na moja sikioni, ndipo akakimbia kwenda jikoni kuokoa maisha yake, huku Musimo akitoweka kwa miguu.

"Yaani ni kwamba dereva wa bodaboda alimfikisha na kuondoka, hivyo baada ya kunikata akakimbia, wanafunzi waliona tukio na kupiga kelele



na kumfuata wakiwa na mwalimu wa zamu na polisi waliokuwa wakisimamia mtihani shuleni kwangu walikimbizana naye na kumkamata," alisema.

Alisema kuwa alichukuliwa na wasimamizi wa mitihani na kupelekwa katika Kituo cha Afya Murangi na kushonwa nyuzi kichwani na sikioni na kuongezwa damu.

"Kesho yake Profesa Muhongo alipiga simu Kituo cha Afya Murangi na kuomba gari la wagonjwa linipeleke Hospitali ya Rufani ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere nililazwa kwa siku tatu," alisema.

Alisema hakujua kwamba atakuwa hai hadi sasa, na kwamba Mungu amemjalia kuendelea kuwa hai, lakini anahofia usalama wake iwapo atarudi Makojo, kwani hajui ni kwanini amefanyiwa ukatili huo.

"Ninawashukuru wasamaria wema wote akiwamo Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, aliyejitolea kulipa gharama zote za siku tatu nilizolazwa hospitalini pamoja na chakula," alisema.

Alifafanua kuwa mbunge huyo pia amemlipia kodi ya nyumba ambayo mwalimu huo anaishi, kwa muda wa miezi mitatu wakati huu ambao anaendelea kuuguza majeraha.

Akizungumzia tukio hilo, Prof. Muhongo alisema lisichukuliwe kama tabia ya watu wa Musoma Vijijini, bali ni vitendo vya mtu mmoja ambaye kwa sasa anashikiliwa na vyombo vya dola.

"Aliyefanya tukio hilo ametutia aibu, lakini niwahakikishie watumishi wanaofanya kazi jimboni mwetu kuwa huyo si kigezo cha kuchafua taswira ya Musoma Vijijini," alisema Prof. Muhongo.

Mbunge huyo alimtaka mwalimu kuwa na amani wakati taratibu nyingine zikiwamo za kumwezesha kuendelea na utumishi wake kwa amani zikiendelea kufanyika.

"Nimeamua kumlipia kodi ya nyumba kwa miezi mitatu huku taratibu nyingine za kuhakikisha anakuwa katika mazingira salama ya kuwahudumia wanafunzi zikiendelea," alisema.

## TANGAZO

**MAJEMBE AUCTION MART KWA MAMLAKA TULIYOPEWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA CHINI YA AKIBA COMMERCIAL BANK PLC** Tutauza Magari ambayo ni mali ya Benki hiyo kwa njia ya Mnada.Taarifa za gari na tarehe ya Mnada huo kama inavyojieleza hapo chini

| JINA LA MMILIKI | NAMBA YA GARI | AINA YA GARI | MAHALI GARI ILIPO | MWAKA WA KUTENGENEZWA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| AKIBA COMMERCIAL BANK LIMITED | T 138 CKF | LANDROVER DISCOVERY 4 | AKIBA BENKI HEAD OFFICE | 2013 | 17/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AKIBA COMMERCIAL BANK LIMITED | T367 BAQ | TOYOTA LANDCRUISER | AKIBA BENKI HEAD OFFICE | 2009 | |
| AKIBA COMMERCIAL BANK LIMITED | T391 BXD | TOYOTA RAV4 | AKIBA BENKI HEAD OFFICE | 2011 | |
| AKIBA COMMERCIAL BANK LIMITED | T973 AYF | TOYOTA HILUX | AKIBA BENKI HEAD OFFICE | 2008 | |
| AKIBA COMMERCIAL BANK LIMITED | T718 DJA | TATA XENON PICK-UP | AKIBA BENKI HEAD OFFICE | 2014 | |
| AKIBA COMMERCIAL BANK PLC | T913 DKG | TATA XENON PICK-UP | AKIBA BENKI TAWI LA ARUSHA | 2013 | |
| AKIBA COMMERCIAL BANK LIMITED | MC768 AEM | HONDA ACE 125 | AKIBA BENKI HEAD OFFICE | 2013 | |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu No.**0715868000/0754301930**

217706902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wazazi wanaooza mabinti wadogo wakomeshwe

**BAADHI** ya wazazi na walezi wamekuwa na tabia ya kuzima ndoto za watoto wao za elimu kwa kuwakatisha masomo na kuwaoza kwa lengo la kupata mahari.

Tamaa ya pesa huwaondoa utu wao na baadhi ya kuwalazimisha kufanya vibaya kwenye mitihani ili wasiendelee na masomo.

Tabia hii imekuwa ikiwaweka mabinti wengi kwenye tatizo kubwa la ukatili wa kijinsia kutokana na umri wao kutohimili vishindo vya kwenye ndoa.

Wengine hupata matatizo kwenye uzazi kutoka na viungo vyao kuwa bado havijakomaa kuhimili ubebaji mimba mpaka kujifungua.

Kutokana na hali hiyo kushamiri, hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, aliwaonya baadhi ya wazazi na walezi wenye tabia kama hiyo kuwa serikali ya mkoa huo haitawavumilia wale wanaochukua posa na kuwaozesha watoto wao badala ya kuwapeleka shuleni.

Mkuu huyo wa mkoa aliona atoe salamu hizo siku alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mabatini, Halmashauri ya Mji Njombe, ambao walikuwa kwenye maandalizi ya mtihani wao wa mwisho.

Aliamua kuzungumzia hilo baada ya kuona mtoto anayelazimishwa kuingia kwenye ndoa akiwa na umri mdogo ambao hawezi kuamua afanye nini kwenye maisha yake.

"Kwamba usinilazimishe mimi mtoto wangu aende shule au asiende, huyu mtoto umri huu anaamua nini, darasa la saba katoto kadogo haka unapokea posa ya kwenda wapi, kwamba umepokea posa ya kwenda wapi hawa watoto, anaenda leba huyu hata kuchumbiwa anachumbiwaje huyu," alihoji Mtaka.

Vile vile, mtu anaweza kushangaa mtu mzima na akili zake timamu anakwenda kukichumbia kitoto ambacho anaweza kukizaa au pengine akawa hata mjukuu wake.

Hii yote inatokana na tamaa za kimwili na kujiondoa ufahamu wa kumkwamisha binti kwenye ndoto yake ya kupata elimu.

Binti anayekwamishwa kimasomo pengine huko mbele angekuja kuwa kiongozi mkubwa katika nchi au mtaaalamu wa jambo fulani linaloweza kuokoa maisha ya watu.

Mtaka amewashauri wazazi wa wanafunzi waliomaliza darasa la saba mwaka huu ambao hawapo tayari kuwapeleka watoto wao shuleni kujiunga na masomo ya sekondari mwakani endapo watafaulu wanatakiwa kuhama Mkoa wa Njombe.

Ameonya kama kuna mzazi ana mtoto nyumbani amemaliza darasa la saba amefaulu kwenda kidato cha kwanza na hana mpango wa kumpeleka ahame huu mkoa na kutoa mfano wa watu zamani walikuwa wanakimbia kodi za kichwa wao watakimbia na nyumba.

Serikali imejenga madarasa na kupeleka madawati na vitabu katika shule zote nchini hivyo hakuna sababu ya mzazi kuacha kumpeleka mtoto wake shuleni.

Miaka ya nyuma tulikuwa tukishuhudia kipindi cha watoto wanapomaliza elimu ya msingi, baadhi ya watu walikuwa wakitegesha ili kwenda kuwalaghai wazazi ili wawape watoto wao waende kuwafanyisha kazi za ndani.


Lakini ulipokuja mpango wa elimu ya bure na shule nyingi kujengwa nchini, kila mtoto sasa hivi anakwenda shule kwa sababu hakuna kisingizio kuwa ameshindwa kusoma kwa sababu ya kukosa nafasi.

Ofisa Elimu Mkoa wa Njombe, Nelasi Mulungu, alisema maandalizi kuelekea mtihani wa taifa kidato cha nne mkoani Njombe yanaendelea vizuri na yalianza tangu wakiwa kidato cha kwanza.

Mkoa wa Njombe umepewa kipaumbele kwenye elimu ili kuhakikisha kiwango kinapanda.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Mary Seme

## Muungwana Lazima Nilonge

# Vituo vya abiria visigeuzwe vijiwe vya kufanya biashara

**IMEKUWA** jambo la kawaida hapa Dar es Salaam, kwa baadhi ya maeneo ya kupumzika abiria kwa ajili ya kusubiri magari, kumegeuzwa kuwa sehemu za ujasiriamali huku baadhi ya abiria wakikosa sehemu za kupumzika.

Jambo hilo linaloota mizizi, si zuri kwani limegeuka na kuwa kero kwa abiria pindi wanapokosa sehemu za kukaa huku wafanyabiashara hao wakiendelea na biashara zao pasi kujali kuwa maeneo hayo si rasmi kwa biashara zao.

Mfano wa maeneo mbalimbali hapa jijini Dar es Salaam ambayo ni vituo vya abiria na vimegezwa kuwa sehemu za biashara ni kama vile, Tabata, Mbezi, Segerea na Kimara, ambako vituo vya maeneo hayo vimegeuzwa na baadhi ya wananchi wasio waadilifu na kuyafanya kuwa ni sehemu ya kujipatia kipato ilhali wakijua fika kuwa sio sehemu sahihi ya wao kufanyia biashara zao, jambo ambalo limekuwa likiwashangaza abiria wanaosubiri magari kwa ajili ya kupanda na kuendelea na safari zao na pengine kuwatolea lugha chafu abiria wanaokaa mbele ya biashara hizo kwamba wanazuia zisionekane vyema kana kwamba wapo sahihi kuweka biashara hapo.

Zipo mamlaka husika zinazoshughulikia masuala ya usalama barabarani mathalani polisi msifumbie macho suala hili kwa kushirikiana pamoja na serikali za mitaa tafuteni ufumbuzi.

Katika kanuni za kufikia ufanisi, daima kila jambo linafaa litumike kwa ajili ya matakwa husika.

Mathalan, nitoe mfano pale utakapokuta gari la kuchukua wagonjwa linatumika kwa shughuli tofauti na utabibu, ni wazi hiyo inaangukia kwenye ubadhirifu.

Hivyo, ni muhimu sasa kwa mamlaka hizi kuliangilia suala hili na kulikomesha kwani ni kero kwa wananchi. Ipo haja ya mamlaka hizi kuliona jambo hili kwa kulitazama kwa jicho la tatu bila kulifumbia macho na kutatua kero hii kwa wakazi wa Jijini hapa.

Kwa kufanya hivyo wafanyabiashara watashituka na kuogopa kufanya biashara zao wakihofia kuvunja sheria na kanuni zilizowekwa na mamlaka husika.

Sheria tayari zipo na haziruhusu watu kufanya biashara maeneo yasiyokuwa rasmi kwa shughuli hizo.

Maeneo haya ambapo shughuli hizi za biashara zimekuwa zikifanyika yamekuwa pia yakisifika kwa kero ya uchafu utokanao na biashara hizo zinazofanyika maeneo haya ambayo siyo rasmi wala sio salama kwa afya ya binadamu. Uchafu huo ni kama vile, mabaki ya matunda yaliyoharibika, makopo ya maji na baadhi ya vyakula vinavyomwagwa na mama lishe wanaouza vyakula vyao katika maeneo haya.

Kwahiyo wafanyabiashara hao wanaogeuza vituo vya daladala kuwa sehemu za kufanyia biashara ni muhimu wajue watachukuliwa hatua za kisheria kwa kukiuka kwao utaratibu uliowekwa na mamlaka husika itasaidia katika kupunguza na kukomesha adha hii.

Mazoea hujenga tabia na kwa hili la wafanyabishara kugeuza vituo kuwa sehemu za biashra limeshaota mizizi, hivyo inahitajika nguvu ya ziada kulidhibiti kabla sasa halijaonekana ni jambo tu la kawaida.

Jambo ninalojiuliza, ni kwamba serikali ya mitaa ipo mpaka hapo kunakotokea mambo hayo; ofisi za vitongoji, kata, diwani na wengine wengi wa ngazi hiyo wanaozunguka mahali hapo, hawayaoni hayo?

Vilevile, tunapotamka mustakabali wa kuwajibika katika wajibu wetu wa kiserikali, hawaoni chochote cha kuchukulia kiserikali ama kutetea au kusawazisha maslahi ya umma katika ngazi ya wajibu wao?

Unapoona miundombinu ya namna yoyote ya umma mbele yako, ni wazi imegharimiwa kwa pesa nyingi sana zitokanazo na kodi zangu, pia za kwako. Katika mantiki hiyo kwanini hatuna ishara ya uchungu katika nafsi zetu, vyote hivyo matumizi yake yawe katika namna chanya kwa kadri makusudi yake yalivyo na kutokutoa nafasi kwa lolote lile lililo hasi, kama hayo tunayoyaona na kuyalalamikia.

Nihitimishe tu kwa sauti, tutambue tulikojikwaa tukiunda safari chanya kwa matumizi ya mali zetu, naamini linawezekana.

## NEMC yatoa tahadhari mafuriko migodini

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewataka wamiliki wa migodi kuchukua tahadhari dhidi ya mafuriko yanayoweza kutokea kwenye mabwawa yao ya kuhifadhia taka sumu.

NEMC imesema wasipochukua tahadhari kuna uwezekano wa mabwawa hayo kufurika na kupasuka, hivyo kusababisha mafuriko kwenye makazi ya watu na hata kusababisha vifo.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu mvua zinazoendelea.

"Mvua kubwa zinaendelea kunyesha na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeshatoa tahadhari na hizi mvua zinaweza kuwa na dharura na majanga ambayo yanaweza kuwa makubwa na kuathiri uhai wa watu na afya zao. Kwa hiyo tumeona ni vyema tukachukua tahadhari badala ya kusubiri maafa ndipo tuseme," alisema.

Alisema wamiliki wa migodi mikubwa na ya kati wamekuwa na kawaida ya kujenga mabwawa ya kuhifadhi taka sumu ambayo huwa yanachukua sehemu kubwa ya ardhi.

"Haya mabwawa ni makubwa sana. Sasa kunapotokea mvua kubwa yanafurika na yakipasuka yanaweza kusababisha madhara makubwa kwa wananchi, hivyo wanapoona dalili za mabwawa yao kufurika watoe taarifa kwa mamlaka husika ili tahadhari zichukuliwe," alisema.

Dk. Gwamaka alisema kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, watu wote wenye mabwawa huwa wanapewa masharti kwa ajili ya kuyatunza kwa tahadhari yasisababishe maafa kwa wananchi.

Alisema wenye mabwawa hayo wanatakiwa kutengeneza mazingira ambayo inapotokea dharura ambayo haikutarajiwa mamlaka husika zipewe taarifa na kuchukua hatua za kuokoa wananchi walio jirani.

"Na wananchi wa maeneo jirani wanapaswa kuelimishwa ili likitokea janga wasipate madhara, nchini kwetu hapa haijawahi kutokea bwawa likapasuka na kusababisha majanga lakini kwingine duniani huko yanatokea mara kwa mara kwa hiyo hatupaswi kukaa kusubiri janga litokee," alisema.

Wakati huo huo, Dk. Gwamaka alisema Desemba 7, wataanza msako kwenye viwanda mbalimbali nchini kukagua kama wana mpango wa kurejeleza chupa za plastiki za rangi ambazo zimekuwa zikichangia uchafuzi wa mazingira.

Alisema katika siku za karibuni chupa hizo za rangi zimekuwa zikitumika kwa wingi na kusababisha uchafuzi wa mazingira na kuchangia kuziba mitaro na mifereji ya maji hasa wakati wa mvua za muda mrefu.

"Nimewasiliana na wanaozitengeneza wanampango gani na chupa hizo, wengine wakasema wanazirejeleza lakini imeonekana kuna viwanda vinaweka vinywaji kwenye hizo chupa lakini hawana mpango wa kuzirejeleza hawa ndio tutawatafuta," alisema.



Mkazi wa Kasamwa, Sumaye Mashaka (34) (aliyefunika uso wake), akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 8 jela na Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita jana, baada ya kukutwa na hatia ya kumuua bila kukusudia kimada wa mume wake, Asha Simba (34). **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Jela miaka 8 kumuua kimada wa mumewe

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi mjini Geita, imemhukumu mkazi wa Kasamwa, Sumaye Mashaka (34), kifungo cha miaka minane jela kwa kosa la kumuua bila kukusudia kimada wa mume wake Asha Simba (34).

Mashaka alitiwa hatiani baada ya kubainika kumwagia mafuta ya petroli kisha kuwasha kibiriti na kumuunguza sehemu mbalimbali za mwili wake na kufariki dunia.

Hukumu hiyo imetolewa na Jaji Lilian Itemba baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa la kumuua bila kukusudia kimada huyo wa mume wake.

Jaji Itemba alisema kwa kuwa mshtakiwa amekiri kosa bila ya kulazimishwa, alimwomba Wakili wa Serikali, Godfrey Odupoy, amsomee maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili Odupoy alidai kuwa mshtakiwa alikuwa akimtuhumu mume wake, Kisa Clement, kwa kuingiza ndani ya nyumba yake vimada eneo la Kasamwa, Wilaya ya Geita.

Wakili huyo alidai kuwa Septemba 25, 2022 majira ya usiku, eneo la Kasamwa, Geita, mshtakiwa alimfumania mume wake ndani ya nyumba yao akiwa na kimada huyo.

Baada ya kuona kitendo hicho, alidai kuwa mshtakiwa alikasirika na kuchukua mafuta ya petroli na kumumwagia Asha kisha kuwasha kibiriti na kumuunguza sehemu mbalimbali za mwili wake.

Alidai kuwa baada ya tukio hilo, mshtakiwa alikimbia na kutokomea kusikojulikana na kumwacha kimada wa mume wake akiwaka moto.

Pia alidai kuwa baada ya tukio hilo, Asha alichukuliwa na wasamaria wema hadi kituo cha polisi Kasamwa na kupewa PF3 kisha kupelekwa katika Kituo cha Afya Kanyara na alipofikishwa hapo, alipewa rufani kwenda kwenda Hospitali ya Bugando, Mwanza kwa matibabu zaidi.

Wakili huyo alidai kuwa Oktoba 8, 2022 Asha alifariki dunia na mwili wake ulifanyiwa uchunguzi na daktari na kubaini kuwa chanzo cha kifo ni majeraha makubwa yaliyokuwa sehemu mbalimbali za mwili wake yalisababishwa na kuunguzwa kwa moto wa petroli.

Aidha, alidai kuwa polisi waliendelea kumsaka mshtakiwa na ilipofika Desemba 12, 2022 mshtakiwa alikamatwa na kupelekwa kituo cha polisi Geita na alipohojiwa, alikiri kumuua bila kukusudia kimada wa mume wake. Upelelezi ulipokamilika, mshtakiwa alipelekwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Wakili huyo aliendelea kudai kuwa juzi mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani na aliposomewa mashtaka, alikiri kumuua bila kukusudia kimada wa mume wake.

Baada ya Wakili Odupoy kumaliza kumsomea maelezo ya awali, Jaji Itemba alisema mahakama inamtia hatiani kwa kosa la kuua bila kukusudia, hivyo kumtaka ajitetee ili apunguziwe adhabu.

Wakili wa Kujitegemea, Penina Mashimba, aliyekuwa akimtetea mshtakiwa huyo, alidai kuwa hilo ni kosa la kwanza kwa mteja wake na pia amejutia kosa lake.

Pia alidai kuwa mteja wake amekaa mahabusu kwa muda wa mwaka mmoja na kwamba mume wake siku ya tukio, mshtakiwa alimkuta akiwa amelala na mwanamke ndani ya nyumba yao na alipomuuliza mume wake majibu yake ndiyo yaliyomfanya afanye kitendo hicho.

Wakili huyo pia alidai kuwa mshtakiwa ana watoto wanne na kwa sasa wanaishi na baba yao, hivyo kuomba mahakama impunguzie adhabu ikiwezekana kifungo cha nje ili awatunze watoto wake.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na mawakili Odupoy, Mussa Mlawa na Verena Mathias, ulidai kuwa hauna kumbukumbu ya makosa ya zamani ya mshtakiwa lakini kitendo alichokifanya ni cha kikatili, hivyo kuomba mahakama itoe adhabu kubwa kwa mujibu wa sheria ili iwe fundisho kwa wanawake wote wanaofanya vitendo hivyo vya kikatili. Jaji Itemba alisema: "Pamoja na kwamba mshtakiwa ulikuwa umepitia changamoto hizo zote za kumkuta marehemu akiwa amejifunga kitenge chako ndani ya nyumba yako na baada ya kitendo hicho ukaenda kuchukuwa mafuta ya petroli na kumumwagia kisha ukawasha kibiriti na kumuunguza na hatimaye ukakimbia, kitendo hicho ni cha kinyama sana.

"Pamoja na kudai kwamba hukukusudia, haya ni mauaji makubwa sana, hivyo mahakama hii inakuhukumu kifungo cha miaka minane jela na rufani iko wazi kwa pande zote kama hamkuridhika na hukumu hii."

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# Jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

MAHAKAMA Ya Hakimu Mkazi Singida, imemhukumu mkazi wa Mtaa wa Kilambida, Kata ya Kindai, Manispaa ya Singida, Daudi Mustafa (27) kifungo cha miaka 30 jela na fidia ya Sh. milioni mbili baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Kindai.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Nuru Chiwalo, alidai kuwa siku ya tukio wakati mwanafunzi akirudi nyumbani, mshtakiwa alimfuata nyuma akitoka sokoni alikotumwa kununua mafuta ya kupikia.

Chiwalo alidai kuwa mwanafunzi huyo, mwenye umri wa miaka 15, alipofika kwenye kichaka kilichokuwa maeneo ya relini, ndipo mshtakiwa alimkamata na kisha kumziba mdomo na kumvua taiti yake pamoja na nguo zake za ndani, naye alivua nguo zake na kuingiza uume wake kwenye sehemu za siri za binti huyo.

"Binti huyo alishindwa kupiga kelele kwa sababu alizibwa mdomo na baada ya mshtakiwa kumaliza kumfanyia unyama, alikimbia na mwanafunzi alikwenda nyumbani kwao huku akiwa analia na kumsimulia dada yake maswahibu yaliyompata," alidai.

Mwanasheria huyo pia alidai kwamba baada ya dada huyo kusimuliwa mkasa huo, alimpeleka mwanafunzi huyo kituo polisi na kupatiwa PF3 kwenda kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida.

Chiwalo alidai kuwa uchunguzi wa daktari ulibaini kwamba mwanafunzi huyo aliingiliwa kutokana na kuonyesha kipenyezo huku akiwa na michubuko lakini hakuwa na magonjwa yoyote aliyoambukizwa na kwamba alipatiwa dawa za kuzuia maradhi ya UKIMWI.

Katika utetezi wake, mshtakiwa huyo alidai kuwa saa ya tukio hilo, hakuwapo kwa kuwa wakati huo alikuwa amelewa na alikuwa amelala nyumbani kwake, ushahidi ambao uliungwa mkono na mashahidi wake wawili ambao aliwapeleka mahakamani hapo.

Pamoja na ushahidi na utetezi huo, Chiwalo alidai kwamba hawakutoa uthibitisho wowote ulioonyesha kwamba wakati wa tukio mshtakiwa alikuwa amelala.

Kabla ya Hakimu kutoa hukumu, mshtakiwa aliomba asamehewe kutokana na kutokuwa na makosa mengine ya siku za nyuma.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mkuu Robert Oguda alisema ili iwe fundisho kwa mshtakiwa na watu wengine wenye tabia kama ya mshtakiwa, anamhukumu kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 30 pamoja na kumlipa mwathirika fidia ya Sh. milioni mbili.

# Katibu Mkuu Uchukuzi ataka Bandari ya Mtwara kutumika

**Na Salome Kitomari**

KATIBU Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kahyarara, amesema uwezo wa Bandari ya Mtwara kwa sasa kupokea shehena ya mizigo ni kubwa na ina mfumo wa kisasa, hivyo amewahamasisha mawakala kutumia fursa hiyo ipasavyo.

Akizungumza jana na wasafirishaji katika mpaka wa Tanzania na Zambia na taarifa yake kupatikana kwa umma, alisema Bandari ya Mtwara inauwezo wa kushusha na kupakia makontena 25 kwa saa, hivyo ni fursa ya kupunguza msongamano Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema kwa mawakala kutumia Bandari ya Mtwara ni faida kubwa kwao kwa kuwa itapunguza umbali wa safari kutoka Dar es Salaam na kuokoa muda wanaoutumia na hivyo kurahisisha biashara kwa pande zote.

Kwa mujibu wa Profesa Kahyarara, Rais Samia Suluhu Hassan alishatoa maelekezo kwa wadau wa korosho kuitumia Bandari ya Mtwara na kwa sasa inasafirisha makaa ya mawe yote yanayokwenda kwenye soko la dunia.

"Wasafirishaji wa mizigo kwenda Zambia na Malawi wataokoa muda mwingi unaotumika hivi sasa kusafiri kwa barabara umbali wa kilomita 800, kwani tayari serikali imeimarisha usafiri kuanzia bandari ya Mtwara mpaka Mbambabay kwenye Ziwa Nyasa," alisema na kuongeza:

"Kutoka katika Bandari hiyo ya Ziwa Nyasa wanaweza kwenda mpaka Malawi Nkatabay au Lilongwe. Hiyo itapunguza umbali wa barabara muda wa safari na gharama.

"Tayari kuna meli tatu katika Ziwa Nyasa mbili za mizigo MV Songea na MV Ruvuma ambazo zinauwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja na meli nyingine MV Mbeya ambayo inauwezo wa kubeba abiria 600 na tani 200 za mizigo."

Katibu Mkuu huyo alisema mikoa ya Songwe, Njombe, Iringa na Mbeya kupitia Ziwa Nyasa wanaweza kupitisha shehena zao Bandari ya Itungi au Kiwira.

"Kama wanakutumia barabara wanaweza kutokea Ruvuma mpaka Njombe, serikali pamoja na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), tuko mbioni kukamilisha tathmini ya muda na gharama yaani 'total Route Cost' itakayotoa gharama na kiasi cha muda utakaookolewa kwa watumiaji bandari ndani na nje," alibainisha.

Aidha, Profesa Kahyarara alisema Rais Samia amedhamiria kuongeza mchango wa sekta ya usafirishaji katika pato la Taifa, ajira na fedha za kigeni kwa namna nyingi ikiwamo kutumia fursa za kijografia kama uwepo wa Bandari ya Mtwara.

Serikali iliwekeza vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuhudumia meli za makasha, na Rais Samia alipotembelea bandari hiyo Septemba mwaka huu, aliagiza korosho zote kusafirishwa kupitia hapo.

Siku chache baadaye, Oktoba 22, mwaka huu, Bandari ya Mtwara ilipokea shehena ya kontena 300 iliyowasili kwa ajili ya kusafirisha korosho ambazo hadi wakati huo tani 20,000 zilishauzwa kwa wanunuzi kutoka nchi mbalimbali.



Diwani wa Kata ya Mlimba, Waraji Abdallah Hassan (wa tatu kushoto), akikata utepe kuzindua rasmi tawi la BRAC, Mlimba mkoani Morogoro juzi. Wengine ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mlimba, Wolfram Mhiche (wa tatu kulia), Meneja wa BRAC Mkoa wa Morogoro, Masha Kabange (wa pili kushoto) na wafanyakazi wengine wa taasisi hiyo na wateja. **PICHA: MPIGAPCHA WETU**

# RC awapa neno wazalishaji wa chumvi

**Na Mwandishi Wetu, MTWARA**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas, amewataka wazalishaji wa chumvi nchini kuzalisha na kuifungasha kwa kuzingatia viwango, ubora na usalama ili kulinda afya za watumiaji.

Kanali Abbas alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo kwa wadau wa chumvi mkoani humo yaliyoandaliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Alisema azma ya serikali ni kujitosheleza kwenye uzalishaji wa bidhaa muhimu kama chumvi, hivyo wadau hao wana wajibu wa kuendelea kuzalisha na kufungasha chumvi iliyo bora.

Alisema mafunzo hayo yamekuja kwa wakati mwafaka na serikali imeazimia kwa dhati kuendeleza viwanda ili kutoa ajira katika kada mbalimbali pamoja na kuziwezesha bidhaa za hapa nchini kushindana katika masoko ya ndani, kikanda na ya kimataifa.

"Kwa hiyo nitoe rai kwenu nyie washiriki wa mafunzo haya, msikilize kwa makini na kuchangia mada ili muweze kupata utaalamu na kuutumia mtakaporejea kwenye shughuli zenu," alisema.

Akifungua mafunzo kama hayo yaliyofanyika wilayani Lindi, Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi, Zuwena Omary, aliwataka washiriki kutumia vizuri fursa hiyo ya mafunzo kwani yanagusa mahitaji yao katika uendeshaji na uboreshaji wa shughuli zao katika sekta ya chumvi.

Aliishukuru TBS kwa maandalizi mazuri ya mafunzo hayo na aliomba utaratibu wa kufanya mafunzo kama hayo kwa wadau wa chumvi uwe endelevu.

Mafunzo hayo yametokana na maombi ya wadau hao kupitia vikao mbalimbali vya kamati jumuishi ya kutatua changamoto za sekta ya chumvi nchini.





# Ubakaji, ulawiti vyazidi kushamiri

Na Jaliwason Jasson,
BABATI

VITENDO vya ubakaji na ulawiti dhidi ya watoto, vimeendelea kuwa tishio katika Mkoa wa Manyara baada ya Jeshi la Polisi, kuitaja wilaya ya Babati kuwa kinara wa matukio hayo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, alisema matukio hayo yaliyoripotiwa kwenye madawati ya jinsia ya polisi, kati ya Januari hadi Oktoba, mwaka huu, yamefikia 27.

"Wilaya inayoongoza kwa matukio ya ukatili ni Babati ambayo ina kesi 15 zinazohusu makosa hayo. Kubaka kosa moja, kunajisi watoto wa kiume watatu na kulawiti wa kike mmoja. Mengine ni kutupa watoto wawili wa kike, shambulio la aibu kwa watoto wawili na kutelekezwa katika familia, watoto sita," alisema.

Aidha, katika wilaya ya Mbulu, idadi ya watoto waliobakwa ni watatu na kulawiti wawili, huku Wilaya ya Hanan'g, ikiwa haina makosa ya namna hiyo.

Katika wilaya ya Kiteto, alisema waliolawitiwa ni watoto wanne, kukoseshwa mwanafunzi masomo, kutokana na wazazi kushindwa kutimiza majukumu yao, mtoto mmoja, wakati Simanjiro yameripotiwa matukio ya kuwapo shambulisho la aibu kwa mtoto mmoja.

Mkuu wa Dawati la Jinsia wa Jeshi la Polisi mkoani hapa, Willness Kimario, alisema chanzo kikuu cha makosa ya ukatili ni ulevi na mila potofu katika jamii.

Alisema kitu kinachosababisha kesi nyingi zimalizwe kienyeji ni wazazi kuendekeza undugu kutokana na matukio hayo kufanywa na ndugu zao na hivyo kulindana.

# Bidhaa Tanzania kuingia nchini Uingereza bila kulipwa ushuru

Na Godfrey Mushi,
ARUSHA

BALOZI wa Tanzania nchini Uingereza, Mbelwa Kairuki, amesema Tanzania itaanza kunufaika na mpango wa kukuza biashara wa serikali ya Uingereza, ujulikanao kama Developing Countries Scheme, ambao utaruhusu asilimia 98 ya bidhaa zake kuingia nchini humo bila kutozwa ushuru.

Pia, amesema tayari ubalozi huo umeweka lengo la watalii kutoka pembe zote za Uingereza, kutoka wastani wa watalii 60,116 hadi 200,000 ndani ya miaka mitatu ifikapo mwaka 2027.

Akizungumza jana na Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) kwa njia ya mtandao, Balozi Kairuki alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi 65 duniani zilizoingizwa katika mpango huo wa Uingereza.

Balozi kairuki alisema kwenye eneo la biashara, mauzo ya bidhaa za Tanzania nchini Uingereza, bado ni madogo na kwamba mwaka jana mauzo yalifikia paundi za Uingereza milioni 49 kulinganisha na Uganda ambayo mauzo yake yalifika paundi milioni 89, huku Kenya mauzo yao yakiwa mara 10 ya mauzo ya Tanzania baada ya kufikia paundi milioni 600.

"Kwa kweli kwa takwimu hizi, ni lazima tujipangue na kujipanga upya kimkakati ili mauzo yetu yaongezeke zaidi, kwa sababu uwezekano huo upo mkubwa sana. Hapa ubalozini tumejiwekea lengo la kuongeza mauzo ya biadhaa za Tanzania ya paundi milioni 49 za mwaka jana, hadi kufikia walau paundi milioni 150 ndani ya miaka miwili ijayo, yaani mwaka 2025.

"Bahati nzuri nchi yetu ni miongoni mwa nchi 65 duniani, ambazo zimeingizwa katika mpango wa kukuza biashara wa serikali ya Uingereza, ujulikanao kama Developing Countries Scheme. Chini ya mpango huu, asilimia 98 ya bidhaa kutoka Tanzania zikiingia hapa Uingereza hazitotozwa ushuru. Hii ndugu zangu ni fursa kubwa sana kwa nchi yetu," alisema."

Kuhusu utalii, Balozi Kairuki alisema Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza tayari umechukua hatua ya kuanzisha dawati mahususi la utalii ubalozini, na kuajiri mtaalam maalum wa masuala ya utalii.

"Aidha, tutaanda Tourism Road Show katika miji mbalimbali ya Uingereza na Ireland ili kuwezesha kukutana na mawakala wa utalii na waendeshaji kampuni za utalii wa hapa Uingereza ili kuwauzia packages za Tanzania na kuwafahamisha wazifahamu.

"Malengo yetu ni kupanua wigo, badala ya kuiuza, kui-promote Northern circuit iliyozoeleka (hifadhi zilizoko kaskazini), Serengeti, Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, Hifadhi ya Taifa ya Arusha, tunataka sasa tu-promote na Southern circuit (hifadhi za kusini) kuanzia Ruaha, Kitulo na maeneo mengine ya kusini ambayo yana vivutio vingi vya utalii.

"Vilevile, tunataka kutangaza ukanda wa magharibi kule Gombe, Kigoma kwenye mbuga nzuri ya Katavi ambayo ina mvuto mkubwa kwa watalii. Vilevile, tutashiriki maonyesho ya utalii na kuanzia kesho (jana), tutakuwa kwenye maonyesho ya kimataifa ya utalii yajulikanayo kama World Travel Matt yanayofanyika hapa London," alisema.

"Katika maonyesho hayo, tunatarajia zaidi ya kampuni 40 kutoka sekta binafsi Tanzania kushiriki. Tunatarajia Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) itatia saini makubaliano na kampuni kubwa kwa ajili ya kutangaza utalii wa Tanzania," alibainisha.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM, Wilaya ya Babati Mjini, mkoani Manyara, Emmanueli Khambay (katikati), akiongoza harambee ya kukusanya fedha kwa ajili ya upanuzi wa Kanisa la Mungu lililopo eneo la Sawe, Kata ya Maisaka hivi karibuni na kupatikana Sh. milioni 20.3. **PICHA: GIFT THADEY**

# Balozi asaka fursa za ajira utalii

Na Mwandiashi Wetu,
ARUSHA

BALOZI Mbelwa Kairuki, amesema ofisi yake inapambana kufa na kupona, kutafuta fursa za ajira katika sekta ya afya nchini Uingereza na Ireland, kwa ajili ya wauguzi 6,000 ambao hawana ajira nchini Tanzania.

Kairuki ambaye ni Balozi wa Tanzania katika mataifa hayo, alisema nchi nyingi za Afrika zimechangamkia fursa hiyo, na wanaoongoza ni Afrika ya Kusini, Nigeria, Zimbabwe na Kenya.

Akizungumza juzi na Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) kwa njia ya mtandao, Balozi Kairuki, alisema Uingereza ziko fursa katika sekta ya afya, ambayo ina mahitaji makubwa ya wauguzi na watumishi wasio na ujuzi (unskilled care givers).

"Takwimu zinaonyesha asilimia 14 ya watumishi wa afya nchini Uingereza wanatoka nje ya nchi.

"Kati ya watumishi wa afya milioni 2.28, watumishi 170,000 ni wageni. Nchi nyingi za Afrika zimechangamkia fursa hii lakini wanaoongoza ni Afrika ya Kusini, Nigeria, Zimbabwe na Kenya.

"Naamini Tanzania tukijipanga, tunaweza kunufaika na fursa hii kwa sababu ninafahamu tuna wauguzi wako takribani 6,000 wako nyumbani, na hawajaingia kwenye ajira. Kwahiyo hawa wanaweza wakachangamkia fursa zilizoko huku Uingereza. Hapa ubalozini tumejiwekea lengo la kutafuta fursa za ajira kwa Watanzania 500 katika kipindi cha miaka mitatu," alisema.

Kuhusu sekta ya elimu, Balozi Kairuki alisema kwa sasa Ubalozi wa Tanzania Uingereza na Ireland, unatafuta fursa za mafunzo na ubalozi utaweka mkazo zaidi katika mafunzo ya sayansi ya afya na teknolojia zinazoibukia.

"Hizi zimepiga hatua kubwa zaidi kwenye maeneo hayo na sisi nyumbani tuna mahitaji makubwa katika fani hizo.

"Nchi yetu ina upungufu mkubwa wa wataalam katika emerging technologies (teknolojia zinazoibukia) katika artificial intelligence (akili bandia), blockchain na software engineers. Nchi inapokuwa na human capital kubwa na yenye ujuzi kwenye tech (teknolojia), ndiyo inakuwa 'mhimili wa uchumi wa kidigitali na biashara zinazoanza.

"Kwenye health sciences (sayansi ya afya), tutafuta fursa za mafunzo kwa wataalam wetu kwenye maeneo tofauti. Tumepanga kuanzisha 'UK-Tanzania Students Conference' itakayokuwa ikifanyika kila mara moja kwa mwaka katika vyuo ambavyo vina idadi kubwa ya Watanzania."

Kwa mujibu wa Balozi Kairuki, lengo la serikali ni kutumia jukwaa hilo kuanzisha mahusiano baina ya Tanzania na vyuo vikuu vya Tanzania na Uingereza.



## Halmashauri yadaiwa kutelekeza miradi inayoanzishwa na wananchi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mkoani hapa, wamelalamikia hatua ya halmashauri kutelekeza na kushindwa kukamilisha miradi mbalimbali inayoanzishwa kwa nguvu za wananchi katika maeneo yao hali inayorudisha nyuma maendeleo katika jamii.

Madiwani hao kutoka kata 26 za halmashauri hiyo walitoa kilio hicho kwa nyakati tofauti wakati wakiwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo katika kata zao wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya mwaka 2023/2024.

Walisema kuwa miradi hiyo ikiwamo ya Afya na Elimu imekuwa ikiachwa katika hatua ya boma huku halmashauri inayotakiwa kumalizia ujenzi ikiitelekeza kwa muda mrefu.

Mmoja wa madiwani hao kutoka Kata ya Bukene, Majaliwa Luhende, alisema kutokana na kero hiyo kubainika katika katika kata zote ni vyema halmashauri kupitia mapato yake ya ndani ikatafuta njia sahihi ya kuhakikisha zinatatuliwa.

"Hili ni tatizo la kata zote tunaomba halmashauri iweke mkakati wa kulimaliza kwa awamu kwa kuanza na zile ambazo wana uwezo nazo kuanza kuzitatua kwani kuendelea kuirundika miradi hii ni kukatisha tamaa wananchi waliowekeza nguvu zao," alisema Luhende.

Kero nyingine zilizowasilishwa na madiwani hao ni ukosefu wa miundombinu ya barabara, maji kutoka Ziwa Victoria, umeme, upungufu wa watumishi, mrundikano wanafunzi darasani, pamoja na mgogoro wa mipaka kati ya Mwakitolyo na Nyanh'wale, Geita.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Nicodemas Simoni, alisema kutokana na changamoto nyingi kujirudia kwa kila kata, aliagiza menejimenti ya halmashauri ianishe changamoto zote ambazo wana uwezo wa kuzitatua kupitia mapato ya ndani.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, David Rwazo, alisema suala la ukamilishwaji wa maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi wataendelea na juhudi za kuyakamilisha kupitia mapato ya ndani, huku akibainisha kuwa maboma 42 wameyakabidhi TAMISEMI kwa ajili ya kusaidia kuyakamilisha.

Kuhusu upungufu wa watumishi tayari limeshaanza kufanyiwa kazi na watumishi 168 wameajiriwa wilayani humo kutoka kanda mbalimbali, huku wakiendelea kuomba maombi ya kupatiwa watumishi wengine na kwa changamoto zingine ambazo zimewasilishwa zitaendelea kutatuliwa kwa kushirikiana na taasisi za serikali.

# Makalla ashtushwa mradi kuongezewa bilioni 11/-

**Na Vitus Audax,** MISUNGWI

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, ameshtushwa na ongezeko la gharama ya Sh. bilioni 11 katika Mradi wa Maji wa Ukiriguru wilayani Misungwi baada ya aliyeshinda tenda kwa Sh. bilioni 21 kukataliwa na kupewa Kampuni ya Emirates kwa gharama ya Sh. bilioni 32.

Kutokana na hatua hiyo, Makalla ametoa siku 14 kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza mradi huo na kubaini sababu za kukataliwa kwa mkandarasi aliyeshinda tenda hiyo awali na kusababisha ongezeko la fedha hiyo.

Alitoa agizo hilo juzi wilayani humo alipokuwa akikagua mradi mkubwa wa maji unaotarajiwa kunufaisha wananchi 85,000 ukiwa na matangi makubwa manne yenye ujazo wa lita milioni 6.5.

"Kwanini mkandarasi Emirates Builders Limited mwenye gharama za juu zaidi ya Sh. bilioni 11 tofauti na mkandarasi aliyeshinda awali apewe kazi hiyo, hapa napata hofu ya ukiukwaji wa sheria na taratibu za zabuni chunguzeni hili na taarifa niipate ndani ya siku 14," alisema Makalla.

Aliwataka Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), makao makuu kutoa ushirikiano kwenye uchunguzi huo kutokana na kusimamia taratibu za kumpata mkandarasi huyo aliyepatikana kwa gharama za juu.

Kadhalika, aliagiza RUWASA kusimamia ipasavyo mradi huo ili ukamilike ndani ya muda uliopangwa wa miaka miwili ili ifikapo Februari 2025 uwe umekabidhiwa.

Alisema serikali tayari imetoa zaidi ya Shilingi bilioni tano kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na sasa umefikia asilimia 12 ya utekelezaji wake hivyo kutaka usimamizi makini wa fedha za serikali.

Katika hatua nyingine alitoa angalizo kwa wananchi kuacha tabia za kujichukulia sheria mkononi kutokana na tukio la kuuawa kwa vijana wawili waliochomwa kupigwa hadi kufa wakiwatuhumu kuiba mpunga na kuku.

Alisema kuwa katika tukio hilo zaidi ya watu 35 wakiwamo viongozi wa kijiji wanashikiliwa na polisi ili kusaidia uchunguzi na maamuzi ya mahakama.



Waandishi wa habari kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa wakiwa na baadhi ya maofisa wa wakala wa barabara nchini (TANROADS), wakikagua ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi, walipofanya ziara ya kujifunza katika mradi huo, jijini Mwanza jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mkandarasi aomba kuongezewa muda wa ujenzi daraja la JPM

**Na Shaban Njia,** MWANZA

MKANDARASI China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC), anayetekeleza ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi maarufu kama Daraja la JPM, ameomba kuongezewa muda wa ukamilishwaji wa mradi huo kutoka Februari 24, 2024 hadi Desemba, 2024.

Meneja wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROAD), Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Paschal Ambrose, alisema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo kwa vyombo vya habari kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Alisema wamepokea maombi kutoka kwa mkandarasi huyo kuongezewa muda wa utekelezaji, lakini bado wanaendelea na mazungumzo naye huku wakimshauri kufanyakazi usiku na mchana ili kufidia muda uliopotea hapo awali kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema mradi huo wenye kilomita 3.2 na barabara za kuunganisha zenye urefu wa kilomita 1.6 unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 716.3, umefikia asilimia 78.06 huku akitaja sababu za uchelewa kuwa ni pamoja na utofauti wa hali ya kijiolojia katika eneo la ujenzi.

Alisema kuwa eneo hilo lilikutwa na miamba mingi kuliko ilivyotarajiwa, vilevile alitaja mvua kubwa iliyonyesha 2019 na kuongeza kina cha maji katika Ziwa Victoria pamoja na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 uliositisha shughuli za usafirishaji wa vifaa kutoka nchini China.

Pia mkandarasi huyo anashirikiana na Kampuni ya Yooshin Engineering Corporation (Korea), Cheil Engineering Co. Ltd (Korea), Rina Consulting S.P. A (Italia) na Afrisa Consulting Ltd (Tanzania) na tayari serikali imemlipa Sh. bilioni 396.310.

Mhandisi msimamizi wa mradi kutoka TANROAD, Abdukarim Majuto alisema, mradi huo utakapokamilika utaunganisha wilaya mbili za Misungwi na Sengerema na kurahisisha kuzifikia nchi za Maziwa Makuu ya Kenya, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

# ama

ALHAMISI NOVEMBA 9, 2023

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**MWAUWASA inavyopambana operesheni kulitakatisha Jiji Mwanza majitaka yatiririke**



Ukurasa 13

AGRA inavyosaidia azma ya serikali kuilisha dunia kupitia mbegu bora



Ukurasa 14

**Ifahamu taasisi inayoangalia madhila ya binti na mama, kuanzia kwenye uzazi**

MAZINGIRA

MAONYESHO YA WIKI MWANAKATAVI...

# Naibu Waziri wa Mifugo atua kunadi kifurushi 'Ufugaji Bora' cha Dk. Samia

- Awapa darasa mwelekeo ng'ombe wao 600,000

**Neema Hussein,** MPANDA

NI siku chache zimepita mkoani Katavi, kulikuwapo na maonyesho ya kila mwaka yanayoitwa Wiki ya Mwanakatavi, ambayo mwasisi wake ni Mkuu wa Mkoa, Mwanamvua Mrindoko, sasa ikiunda mjumuiko kitaifa wa mwaka wa pili mfululizo, tangu kuanzishwa.

Hiyo inagusa zaidi miradi ya maendeleo kimkoa, huku sehemu mojawapo ya vigezo vya kiuchumi kwa mkoa ni ufugaji, ikiwamo ng'ombe na samaki.

Ni vitega uchumi ambavyo tayari kuna maelekezo ya kisera ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, sasa ikinadiwa kila kona kuongozwa na Mtendaji Mkuu serikalini, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anayehimiza mifugo kidogo, inayotunzwa kwa stadi za kisasa.

Mbali na ufugaji ambao uko juu kitaifa, pia kuna vigezo vingine vya kiuchumi mkoani humo vinavyojumuisha kilimo, hifadhi za kitalii na biashara. Mkuu wa Mkoa Mrindoko, katika taarifa yake anafafanua:

"Mkoa wa Katavi tuna ng'ombe zaidi ya laki tisa, mbuzi zaidi ya laki moja, kondoo zaidi ya elfu 59, nguruwe elfu kumi na saba, kuku zaidi ya laki saba, bata zaidi ya elfu 44, punda zaidi ya elfu moja, njiwa zaidi ya elfu 26, kanga zaidi ya elfu moja, sungura zaidi ya elfu moja,"

Vigezo hivyo vya maendeleo,



Viongozi Wizara ya Kilimo, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanahawa Mrindoko na timu yake, wakizuru maonyesho ya Wiki ya Mwanakatavi, siku chache zilizopita mjini Mpanda. **PICHA: NEMA HUSSEIN**

uendeshaji wake unaingia katika dondoo za maelekezo ya Rais Dk. Samia, anayedai mageuzi katika ufugaji nchini kuwa kisasa, mifugo kidogo, lakini yenye tija zaidi.

Hilo linahimizwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye Machi mwaka huu alipokuwa Handeni mkoani Tanga, akasisitiza utekelezaji wa maelekezo ya Rais Dk. Samia katika ufugaji kisasa.

"Serikali hii imesema eneo la Msomera (Handeni) litakuwa eneo la mfano kwa ufugaji wa kisasa na wa kibiashara. Kwa hiyo, ni lazima tuweke utaratibu wa kufanya lionekane ni eneo la ufugaji wa kisasa," anatamka Majaliwa.

"Wizara ya Mifugo pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI tengenezeni taratibu za kuonyesha mfugaji wa Msomera mwenye ng'ombe 70 anafuga kwa tija zaidi kuliko mwenye ng'ombe 300. Hii inaweza kutumika hata kwenye mikoa mingine ambako kuna wafugaji," anasisitiza Majaliwa.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mifugo ma Uvuvi, aina hiyo ya ufugaji ambayo maelekezo ya Rais yanafika pia kwenye samaki, akitaja mwitikio wa Rais kiutendaji, serikali imeunda kinachoitwa Programu Samia Ufugaji kwa Tija (SAUTI)

Akaziagiza Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na Wizara ya Mifugo, ziweke utaratibu utakaowafanya wafugaji wafuge kitaalamu, badala ya utaratibu wa mtu kuwa na mifugo mingi, halafu anashindwa kuhudumia, akiutaja utaratibu unakosa tija.

**WIKI MWANA KATAVI**

Miezi saba baada ya Majaliwa kuagiza ufugaji bora Handeni, mnamo Oktoba 26 katika maonyesho ya Wiki ya Mwana Katavi mjini Mpanda, ilikuwa siku maalum ya Mifugo, Uvuvi na Lishe, mgeni rasmi wa siku akawa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Alexander Mnyeti.

Hapo akawa na maelekezo ya kiserikali kuhusu Dira ya Rais Dk. Samia na mkakati wa wizara yake, ikiwamo SAUTI, akitamka: "Serikali kupitia wizara hii tumeendelea kuhamasisha ufugaji wa kisasa.

"Katavi ni miongoni mwa maeneo ambayo bado yana ufugaji holela, ufugaji usiokuwa na tija, ufugaji ambao ng'ombe hawana mwenyewe, wakiamka asubuhi hawaelewi wanakwenda kula wapi nyasi.

INAENDELEA UK.14

MAZINGIRA

# MWAUWASA inavyopambana operesheni kulitakatisha Jiji Mwanza majitaka yatiririke

• Yawekeza mabilioni kuwezesha mifumo inayowezesha



Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mwanza, Leonard Msenyele, akifafanua jambo kwa ujumbe wa Benki ya Maendeleo Ujerumani, katika mabwawa ya majitaka ya Butuja, jijini Mwanza. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA), sasa inafanya upanuzi mradi wa mabwawa makubwa manne ya majitaka eneo la Butuja Sabasaba, Ilemela, ili kuongeza ubora wa kiwango cha uchakataji maji hayo, kabla hayajaruhusiwa kitaalamu kuingia ziwani.

Majitaka kwa lugha rahisi ni maji machafu ya vyooni, bafuni, kufulia, kuosha vyombo, ambayo ni hatarishi kwa afya ya binadamu yasipotafutiwa mfumo maaalum, wa kuyahifadhi au kuyasafirisha kwenda sehemu rasmi inayotakiwa.

Mhandisi wa Kitengo cha Miradi Majisafi na Majitaka jijini Mwanza, kutoka MWAUWASA, Nuhu Msuya, anaeleza kuhusu utekelezaji wa mradi huo, akitamka:

"Tufanye upanuzi wa ujenzi wa mabwawa makubwa mapya manne ya majitaka, mradi huo umefadhiliwa na Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ulaya (EIB) kupitia Shirika la Maendeleo nchini Ufaransa(AFD), tukitarajia kukamilika ujenzi wake mwaka huu 2023."

Msuya anafafanua kuwa upanuzi wa mradi huo unajumuisha mradi mwingine wa bwawa la majitaka unaojengwa katika Gereza la Butimba jijini hapa, itakaogharimu kiasi cha shilingi bilioni sita utakapokamilika.

Anasema, kati ya fedha hizo,

> **Miaka mitatu ijayo, tunatarajia kuanza upanuzi tena ujenzi wa mabwawa mengine eneo hilo la Butuja na wakazi waliopo jirani kuondolewa na kulipwa fidia.**

mradi wa bwawa la Majitaka Gereza la Butimba pekee, utagharimu shilingi bilioni 2.3, mkandarasi akiwa Mtanzania kwa kushirikiana na Ujerumani unaotarajiwa kukamilika mwezi Januari mwakani 2024 ulioanza kujengwa Juni 2023.

Upanuzi wa mabwawa hayo, unatokana na mahitaji baada yale ya zamani yaliyopo 13 yamezidiwa uwezo wa kuchakata majitaka na uzalishaji.

#### MHANDISI MAZINGIRA

Mhandisi Mazingira wa Mamlaka hiyo jijini Mwanza, Rashid Samli, anaeleza kuwa mfumo wa majitaka katika jiji hilo mtandao wake ni kilomita 147.29, ambao umehusisha maeneo mbalimbali, ambayo ni Igogo, Mjini Kati, Mabatini Isamilo, Kirumba, Kilimahewa, Kitangiri, Kabuhoro, Pasiansi, Igogo Kusini na Bugando, Mwanza.

Anasema mtandao wake ulirithiwa kutoka Halmashauri ya Jiji hilo mwaka 1998, baada ya kuanzishwa Mamlaka za maji chini ya Wizara ya Maji na Mifugo enzi hizo.

Mhandisi Samli anaeleza kuwa, kazi kubwa ya mfumo huo Mwauwasa ni kukusanya majitaka kutoka majumbani na kuyapeleka katika mabwawa hayo ya Butuja Ilemela, kwa ajili ya kuyatibu ili kufikia kiwango cha kuwa majisafi na salama baadaye kuyaruhusu kuingia Ziwa Victoria.

Hapo panaelezwa kuwapo jopo la wataalamu wanaotibu majitaka kutoka Mwauwasa na kuyaruhusu kwenda ziwani kwa kushirikiana na Bodi ya Bonde la Ziwa Victoria, kila akiwajibika mtaalamu anayechukua sampuli za majitaka na kuyahakiki ubora uliokusudiwa yakiwa kwenye mabwawa hayo, kabla ya yakuruhusiwa kwenda ziwani.

Sambamba na hilo, inaelezwa kutolewa huduma za uondoshaji majitaka kwa kutumia magari maalum, katika maeneo ambayo mtandao wao haujafika au umefika lakini wananchi hawajaunganishwa kwenye mfumo wa mtandao wenyewe.

"Vilevile tunatoa elimu ya kuwaunganisha wateja katika mtandao wa majitaka, ili kuhakikisha Jiji la Mwanza linakuwa safi na salama, pia MWAUWASA kupitia serikali nchini tumekuwa tukitekeleza miradi ya mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka, milimani katika makazi ya waishio milimani," anatamka Samli.

#### CHANGAMOTO MILIMANI

Hapo anataja milimani kuwapo changamoto kubwa ya wakazi waishio milimani ambayo ni ugumu wa uchimbaji vyoo kutokana na miamba ya mawe, hivyo wakati wa mvua wananchi hao hutiririsha vyoo vyao kushuka chini ya milima na kusababsha kero au kuhatarisha afya za watu wengine wenye makazi chini ya milima.

Hatua inayofikiwa, inatajwa na MWAUWASA, imekamilisha miradi zaidi ya minane katika mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka milimani jijini Mwanza, ilikuwa safi kimazingira katika maeneo ya Sahara, Isamilo, Igogo, Mabatini A na B Kabuhoro, Ibungilo, Kilimahewa, A na B, Pasiansi pamoja na Bugando Jeshini.

#### CHANGAMOTO ZILIZOMEA

Anataja changamoto mojawapop iliyopo ni matumizi yasiyo sahihi ya mfumo wa majitaka kwa wateja, ambao umesanifiwa rasmi kupitisha majitaka tu, lakini wateja waliounganishwa wamekuwa wakiharibu mfumo huo kwa kupitisha taka na kusababisha kuziba mara kwa mara.

Pia anaorodhesha kuwapo wizi wa mifuniko ya 'chemba' za majitaka, kuharibu miundombinu yake kuiba nondo zilizotumika kujengea chemba hizo, raia wasio wema kutupa taka ngumu katika chemba zake wakigeuza dampo, mfano miti, mawe, majani, redi na uchafu mwingine, ikiwamo wananchi wanapokuwa wakifanya usafi.

Vilevile lingine, ni wateja wengine wanatajwa kujiunganishia maji ya mvua kwenye mfumo huo, wakitoboa mabomba yake ili majitaka yaweze kusafirishwa na maji ya Mvua.

#### JUKUMU LA MWAUWASA

Kutokana na changamoto hizo, Mamlaka ya Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza, (MWAUWASA), imekuwa ikichukua hatua kutoa elimu kwa wateja na wananchi juu ya matumizi bora ya mfumo huo, jamii kushiriki mikutano ya serikali za mitaa, ili kupata elimu sahihi ya kudhibiti uzibaji taka mabomba hayo.

Mkurugenzi wa MWAUWASA, Mhandisi Robert Lupoja, anafafanua kuwa upanuzi huo wa mabwawa ya majitaka Butuja Sabasaba umetokana na mabwawa 13 yaliyopo ya zamani ambayo yana uwezo wa kuchakata au kuzalisha lita milioni saba za majitaka.

Mhandisi Lupoja anasema, hivi sasa mabwawa manne yanayojengwa yakikamilika, yatakuwa na uwezo mkubwa zaidi kuzalisha lita milioni 10 sawa na asilimia 30 ya mahitaji na kufikia mwaka 2030 baada ya kukamilika ujenzi huo wa mabwawa, watahamia utekelezaji wa miradi mingine.

"Miaka mitatu ijayo, tunatarajia kuanza upanuzi tena ujenzi wa mabwawa mengine eneo hilo la Butuja na wakazi waliopo jirani kuondolewa na kulipwa fidia. Sasa tuko katika mchakato huo," anasema Mhandisi Lupoja.

Hapo Mhandisi Lupoja anatoa rai, akisisitiza kuwa, wananchi wanatakiwa kutumia vizuri miundombinu ya majisafi na majitaka, badala ya kuiharibu, kutupa uchafu kwenye mifumo yake kama vile pampasi, pedi, mawe, majani na miti inayogeuka kuwa kero kwa watumiaji katika jamii na kusababisha kuziba mifumo ya maji.

MAZINGIRA

# AGRA inavyosaidia azma ya serikali kuilisha dunia kupitia mbegu bora

**Na Mwandishi Wetu**

ILI serikali itimize azma ya Tanzania kuilisha dunia, wadau wa sekta ya kilimo wana mchango mkubwa kufanikisha kwa kuweka mipango thabiti ya matumizi ya mbegu zilizoboreshwa na teknolojia ya kisasa katika kilimo.

Kilimo cha mbegu ni muhimu kwa kuwa mbegu ni chanzo cha uhai, nishati, chakula na dawa. Pia, mbegu ni chanzo cha malighafi za viwandani na mapato ya fedha za kigeni.

Kwa kuzingatia hilo, mbegu zilizoboreshwa ni muhimu ili kupata mavuno ya kutosha na kukabiliana na magonjwa, wadudu waharibifu, ukame, magugu, pamoja na changamoto zingine za mazingira, zikiwamo mabadiliko ya tabianchi.

Hadi sasa nchini kuna Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), inayohusika na utafiti, ubunifu, pia uzalishaji wa mbegu nchini.

Pia kuna Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), iliyoanzishwa mwaka 2003, ikiwa na jukumu la kuthibitisha na kukuza mbegu bora za kilimo zinazozalishwa au zinazoingizwa nchini, kwa ajili ya kuuzwa na kulinda jamii ya wakulima dhidi ya mbegu duni kutoka kwa wauzaji wa pembejeo za kilimo, ikiwa na makoa makuu yake katika Manispaa ya Morogoro na matawi manne yaliyopo; Tengeru (Arusha), Maheve (Njombe), Ukiriguru (Mwanza) na Naliendele (Mtwara).



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima (aliyeinama), akikagua mbegu bora za michikichi, chini ya usimamizi wa Taasisi za Wakala wa Mbegu za Kilimo - ASA na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania – TARI, mkoani humo, Juni mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### SAFARI YA ASA

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Hayati Kofi Annan, alianzisha taasisi inayojishughulisha na ukuzaji wa kilimo Afrika (AGRA) mwaka 2006, ili kuboresha maisha ya wakulima wadogo wa Afrika wanaohangaika na kilimo cha kujikimu na kuwafanya walime kilimo cha biashara.

Maono hayo ya mwasisi wa AGRA, Hayati Annan yameigusa Tanzania kupitia taasisi hiyo iliyopo kwenye mataifa kadhaa ya Afrika, ikishirikiana na serikali, wadau wa kilimo na wakulima katika kuhamasisha kilimo cha kisasa, matumizi ya mbegu zilizoboreshwa na kuwa na soko la chakula lenye ushindani Afrika.

Ofisa Programu ya Mifumo ya Mbegu wa AGRA, Ipyana Mwakasaka, anasema taasisi hiyo imesaidia kuwawezesha watafiti nchini kubuni na kuja na aina mbalimbali za mbegu takriban 44 za mazao mbalimbali, kama vile mahindi, mpunga, maharage soya, mihogo na mengineyo.

"Kati ya mbegu hizo 44 ambazo AGRA imewasaidia watafiti kufanya utafiti na kubuni mbegu, aina 30 ya mbegu hizo zimeshaingia sokoni, baada ya kuidhinishwa na waziri mwenye dhamana ya kilimo na zinafanya kazi vizuri katika mikoa mbalimbali," anasema Mwakasaka.

Anafafanua AGRA pia imesaidia kuanzisha na kuziimarisha kampuni 15 za mbegu nchini, katika kuzalisha asilimia 75 ya mbegu nchini, ili kuepuka na athari za kutegemea mbegu kutoka nje ya nchi.

"Kampuni hizo binafsi 15 za uzalishaji mbegu zilizopata msaada wa AGRA zimefanikiwa kuzalisha mbegu zenye ubora wa hali ya juu zinazofikia ujazo wa tani mita mraba 35,000," anasema Mwakasaka na kuongeza: "Uzalishaji wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi kufikia tani 71,000 mwaka 2020."

Mwakasaka anasema, kumekuwapo mafanikio ya kuongezeka uzalishaji wa mbegu nchini, kutoka chini ya asilimia 20 mwaka 2006, hadi kufikia uzalishaji wa mbegu unaozidi zaidi ya asilimia 60 kwa sasa.

Katika kukabiliana na upungufu wa maofisa ugani, AGRA inasema imetoa mafunzo kwa wakulima viongozi 5,000 wanaowahudumia wakulima wapatao 100 hadi 200, kwa kusaidiana na Maofisa Ugani Kata, katika kupeleka taarifa za kilimo kwa wakulima.

AGRA, pia inahusika katika kusaidia sera za pamoja na mazingira bora ya kilimo nchini, kwa kufanikisha kuandikishwa serikalini kwa mbegu za aina mbalimbali zilizoboreshwa, pamoja na kuondoa ada ya uandikishaji.

### CHANGAMOTO ZILIZOPO

Licha ya mafanikio hayo, bado inatajwa Tanzania inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mbegu zilizoboreshwa, pamoja na kuzalisha asilimia 60, kuna asilimia 40 nchi inaagiza nje ya nchi, hususan kwenye mbegu za mahindi, lakini kwenye mazao mengine ni zaidi ya asilimia 90.

Changamoto hiyo pia inaelezwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Wafanyabiashara ya Mbegu Tanzania (TASTA), Bob Shuma, kuwa asilimia kubwa ya mbegu za 'hybrid' zinazotumika nchini zinazalishwa kutoka nje ya nchi.

"Mbegu zote za 'hybrid' zinazoletwa kutoka nje haziji tu na wala sio msaada, bali zinanunuliwa kwa fedha za kigeni ndipo mnunuzi aende kununua kama ni Zimbabwe ama Zambia," anasema Shuma.

Anaongeza: "Bado inatakiwa kulipa kodi kadhaa na ndio maana zinauzwa bei ghali, lakini kwa mfano sasa kuna uhaba wa dola (fedha za kigeni), tafsiri yake ni nini tutakapo kosa dola mbegu zitakosekana, kama hatuzalishi mbegu sisi wenyewe za kutosha kuna hatari."

Pia, anasema wanajitahidi kusaidia kuhakikisha kunakuwapo sera nzuri, kwani ardhi zipo safi, akitoa mfano wa maeneo yatakayotengwa kwa kilimo cha umwagiliaji, mbegu aina ya 'hybrid' zinapaswa kuzalisha huko huko.

> **Leo tusingekuwa tunakula mahindi, kusingekuwa na utafiti wa mbegu, kwani mahindi yemetokana na tafiti iliyofanywa kutoka kwenye 'Mexican grass' (majani ya Mexico) kwenye karne ya 16.**

"Tuna mabonde mazuri ambayo yamezungumzwa yapo, hayo mabonde mimi nina nia ya kuyataja tuyafanya yawe chini ya serikali, lakini yatolewe kwa ajili ya kuzalishia mbegu za 'hybrid' kwa njia ya umwagiliaji," anatamka Shuma.

Anafafanua kuwa, ili kuzalisha mbegu hizo za 'hybrid' sheria ya TOSCI inatamka mtu anatakiwa kuwa na nafasi ya mita za mraba 400 na hakutakiwi kulimwa mahindi katika eneo hilo.

"Kwa hiyo ardhi tulio nayo lazima tuwe za sera nzuri. Kule tunapoenda kununua mbegu za 'hybrid' wamefanya hivyo. Sisi tusipofanya hivyo, tutaendelea kununua huko mbegu hizo," anasema Shuma.

Pamoja na changamoto za upungufu wa mbegu, mabadiliko ya tabianchi nayo yameelezwa kuchangia kuangamiza mbegu nyingi za asili nchini, kutokana na kushindwa kuhimili mabadiliko hayo.

Ofisa wa Taasisi ya Agri Experience, Dk. Emmarold Mneney, anazungumia changamoto za mabadiliko ya tabianchi inayosababisha kutokea ukame, mafuriko, joto kali, kuibuka kwa magonjwa mapya na wadudu wanaoathiri mbegu hizo.

Dk. Mneney anasema, wanachofanya sasa watafiti wanaozalisha mbegu zilizoboreshwa, ni kurudi katika mbegu za asili kuzizidishia nguvu ili ziweze kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

### HISTORIA YA MBEGU

Akielezea historia ya utafiti wa mbegu duniani, Dk. Mneney anaeleza kwamba, ndio uliosaidia kupatikana kwa mbegu ya mahindi kwenye majani ya ardji ya nchini Mexico 'Mexican grass' na kuboreshwa hata kupatikana mahindi yanayoliwa sasa.

"Leo tusingekuwa tunakula mahindi, kusingekuwa na utafiti wa mbegu, kwani mahindi yemetokana na tafiti iliyofanywa kutoka kwenye 'Mexican grass' (majani ya Mexico) kwenye karne ya 16," anasema Dk. Mneney.

Anasema, mbegu zilizoboreshwa ni ufumbuzi utakaoendelea kuwapo duniani, katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, pamoja na kuboresha uzalishaji wa mazao ili kuendana na wakati.

Dk. Mneney anahitimisha kuwa, mafanikio ya azma ya Tanzania kuilisha dunia yatafikiwa, iwapo tu serikali itaongeza bajeti ya kilimo na kuwekeza zaidi kwenye utafiti wa uzalishaji wa mbegu zilizoboreshwa.

AFYA

# Ifahamu taasisi inayoangalia madhila binti na mama, kuanzia kwenye uzazi

**Na Pilly Kigome**

KATIKA kuleta usawa katika jamii ikiwamo kiafya, taasisi iitwayo Asma Ally Hassan Mwinyi Foundation, imebuni utaratibu wa kumsaidia mwanamke na mtoto katika changamoto zinazowakabili katika maisha yao ya kila siku.

Akielezea undani taasisi katika sekta hiyo, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Asma Mwinyi, anaiambia Nipashe kuwa, sasa wanakabiliana kuangalia uhitaji katika jamii, kwa kujikita kumsaidia mwanamke na mtoto na changamoto zao katika maisha yao ya kila siku.

Asma anasema, harakati hizo zilianza mwaka 2019 kwa usajili uliobarikiwa na Wizara ya Afya, wakianza kumwangalia mwanamke na mtoto wa kike pekee, lakini sasa taasisi hiyo inajumuisha watu wote wenye uhitaji tajwa.

Pia anafafanua kwamba, kwa mtoto wa kike wanawasuka kwa kuwapa elimu ya kijinsia, kisheria na utambuzi shuleni.

Mbali na kutoa elimu hizo, pia wanajikita katika kuisaidia jamii kwa wale wenye mahitaji maalumu Tanzania Bara na Visiwani.

Anafafanua shughuli wanazofanya, wamejikita katika maeneo makubwa matano; Mpango wa Mkoba wa Mama uliozinduliwa Machi 8, mwaka huu, Siku ya Mwanamke Duniani, ambao tayari umeshaokoa watu 600 wa Bara na Visiwani.

Ni mkoba wenye vifaa tiba muhimu vya mwanamke, anapoenda wodini kujifungua, ukisambazwa kwa kumgawia mwanamke, ambaye yuko tayari kaenda kujifungua, lakini kwa bahati mbaya hana vifaa hivyo, ikiwamo sababu ya uchumi duni.

Asma anasema, taasisi yake imekuwa ikipita hospitalini na majumbani, ikiwatumia wenyeviti wa serikali za mtaa, kijiji, vitongoji, wauguzi na wakunga kuwapata wahitaji hao, kwani hao ndio wenyeji wanaofahamu mazingira na wahitaji wao.

"Wakati mwingine tunaenda moja kwa moja hospitali husika kwa wanawake wanaofika kwenda kujifungua na hawana kifaa chochote mkononi, tunalazimika kupelekea huduma hiyo kwa kuokoa maisha ya mama na mtoto," anasema.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (katikati), Asma Allt Mwinyi, akigawa taulo za kike katika Gereza Kuu la Zanzibar. **PICHA: PILLY KIGOME**

Pia katika wanachoiita "Mpango wa Ugawaji Taulo kwa Watoto wa Kike Shuleni na Wanawake walioko Magerezaji (wafungwa)," unaendeshwa kwa kuwaangalia zaidi wanafunzi wenye mahitaji, hasa nje ya mijini na wafungwa magerezani, jumla ya walengwa wanufaika 6000 wameshafikiwa.

Tatu, inatajwa eneo la uchimbaji visima, unaoujumuisha kuchimbaji visima shuleni, kwenye nyumba za ibada, sokoni, vijijini, mpango unaoenda sambamba na kuwapatia matundu ya vyoo katika maeneo hayo.

Anafafanua hadi sasa tayari wameshaokoa maisha ya wanafunzi wapatao 7,777 katika shule mbili zilizopo Unguja, eneo la Pwani Mchangani ambao walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji, pia matundu ya vyoo wakijisaidia porini.

Hapo Asma nataja wamepata matundu sita, ikiwamo kuwapatia matundu misikiti sita ambayo ilikuwa pia haina huduma ya vyoo.

Nne, anadokezea jukumu analolitaja 'kuwafariji wagonjwa majumbani na hospitalini'. Huo anautaja kuwa mpango unaowalenga wagonjwa wote waliotelekezwa hospitalini na wenye hali duni majumbani, wasio na pesa za kujitibu kutokana na uwezo duni wa kifedha au wametelekezwa na ndugu na jamaa.

Asma anasimulia Nipashe kwamba, mpango huo ni endelevu, umekuwapo kwa wagonjwa wenye mahitaji maalum, wamekuwa wakipita kwa kuuona uongozi husika wa hospitalini na kupewa mwongozo kwa wagonjwa wenye uhitaji, hivyo wanawafariji kwa fedha za matibabu na kujikimu, pia vyakula wanapokuwa hospitalini.

Pia anaeleza namna mpango unavyogusa ugawaji wa nguo, vyakula kwa wenye mahitaji majumbani na wana hali duni zilizopitiliza, ikiwamo ugawaji viatu kwa wanafunzi shule za msingi, wenye mahitaji wakiwa katika hali mbaya.

Aina hiyo ya msaada anautaja kujumuisha ugawaji mahitaji ya kumsitiri anayefariki ama nyumbani au hospitalini, kwani kumekuwapo wimbi la uhitaji huo katika maeneo hayo, wanandugu au jamii kushindwa kununua nguo hizo, kutokana na changamoto na ukosefu wa fedha zinazohitajika.

"Tunafanya hivi, kwani nguo hiyo ni muhimu sana, kila mwanadamu anatakiwa astirike pindi anapokwenda kuhifadhiwa katika nyumba yake ya milele. Tunawatumia wajumbe wa mashina, vijiji, au mtaa kuwapata wenye changamoto hiyo" anatamka Asma.

Eneo la tano la jukumu lao katika mustakabali wa kijinsia, unaoitwa 'Mpango wa GBV-Usawa Jinsia' ulioanzishwa mwaka jana, ukijikita zaidi kupinga rushwa ya ngono kwa watoto wasichana shuleni na wanawake wengineo katika rushwa ya ngono.

Ni mpango unaolenga kuwaelimisha wasichana, kuhusiana na rushwa hiyo, wakiwafundisha kuikabili, hata kuepuka rushwa wakiwapa njia wanafunzi wa kike kuepukana na hilo, wasiharibiwe maisha na ndoto zao za maisha yao.

Asma anaeleza, ni aina ya rushwa inayoweza kumfanya mtoto wa kike shuleni akakosa fursa ya kuendelea na masomo au kupata magonjwa ambukizi kutoka kwa walimu au wengine katika jamii inayowazunguka.

"Wote tunajua kuwa rushwa ya ngono haikubaliki katika jamii, hivyo tuna wajibu hasa wa kuwapa elimu watoto wa kike shuleni, vyuoni na kwingineko kuwa jambo hilo halikubaliki," anatamka Asma.

Anataja katika dhana ya kuelimisha jamii, hawajawaacha nyuma wavulana, wanachukua hatua kuwaelimisha kuhusu nadharia zinazohusu hedhi, wakiwapa melekezo namna ya kuwaaidia dada zao, bada ya utamaduni wa kuwacheka kumcheka shuleni.

Vilevile, anaitaja taasisi yake inabeba jukumu la kuwagusa wasio wagonjwa na wahitaji wa huduma zingine kama za uzazi, wakiwapatia mitaji wasiojiweza, wenye hali duni na kuwawezesha kupata mitaji midogo, wapate fedha za kujikimu katika familia zao.

Hiyo ni pamoja na kuwapa elimu za ufundi kwa mabinti wanaokosa kuendelea na masomo kwa kukosa ada au sababu zingine.

Tayari wasichana wasiopungua 19 Zanzibar na Bara wamepatiwa elimu tofauti za ufundi wa cherahani na wamepatiwa mashine hizo, ili wajikwamue kiuchumi.

Hapo Asma ana wito kwa watu wenye uwezo, kusaidia jamii inayowazunguka, akiwa na neno la kuhitimisha: 'Kila mmoja wetu ana wajibu wa kuisaidia jamiii ...'

## Naibu Waziri Mifugo atua kunadi kifurushi 'Ufugaji Bora' cha Dk. Samia

**INATOKA UK.11**

"Katavi ni miongoni mwa maeneo ambayo bado yana ufugaji holela, ufugaji usiokuwa na tija, ufugaji ambao ng'ombe hawana mwenyewe, wakiamka asubuhi hawaelewi wanakwenda kula wapi nyasi.

"Popote mfugaji anapoona kuna nyasi anaingiza ng'ombe wake, sababu ameona kuna nyasi. Wizara ya Mifugo imeendelea kusisitiza wafugaji wote mnaonisikia kuanza utaratibu wa kuboresha ng'ombe wenu, ili mwondokane na utaratibu wa kuswaga ng'ombe na kuchunga kienyeji kama zamani.

"Tunataka tuboreshe, ng'ombe wachache wenye faida kubwa, ambao watakuwa na tija kwenye pato la taifa. Kwa sasa, wizara inahamasisha sana ufugaji wa samaki, wana mchango mkubwa sana kwenye kuondoa udumavu.

"Kwa sababu samaki kama alivyo yeye, ana protini ukimtumia na ndio tunahamasisha wazalishwe kwa wingi na watumike kwa wingi. Sasa wizara imekuja na mkakati wa kufuga samaki kwa njia mbili.

"Njia ya kwanza ni ufugaji wa vizimba na ufugaji wa mabwawa. Vizimba ni lazima ufanyie ziwani, lakini mabwawa unaweza fugia hata nyumbani kwako au shambani kwako, ukatengeneza mabwawa. Ila kwa maelekezo ya wataalamu wetu."

Mkuu wa Mkoa Mwanamvua, anaunga mkono hoja ya Waziri, akiwa na msisitizo wake: "Naomba mzitumie vizuri fursa hizi zilizopo hapa kujielimisha kuhusu kilimo, mifugo, ufugaji wa nyuki, ufugaji wa samaki..."



## Wizara Ardhi kusaidia wananchi popote kupitia mtandao

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ipo kwenye mchakato wa kuanzisha programu tumizi (Ardhi App) ili kurahisha wananchi kupata huduma popote nchini kwa njia ya mtandao.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Anthony Sanga, aliyasema hayo jana kwenye kliniki ya ardhi inayoendelea jijini hapa ya kusikiliza na kutatua kero za ardhi.

Alisema programu hiyo pamoja na mambo mengine itasaidia wananchi kupata huduma ya ulipaji wa pango ya ardhi popote walipo.

Alisema kliniki ya ardhi inayoendelea kwa wiki mbili jijini Dodoma, itakuwa mwarobaini wa changamoto nyingi za ardhi zinazowakabili wananchi wengi.

"Jiji la Dodoma ndio lenye changamoto nyingi za mgogoro ya ardhi na wizara imejipanga kikamilifu kwa kupiga kambi ya wiki mbili ili kuhakikisha changamoto zote za ardhi Mkoa wa Dodoma zinapatiwa ufumbuzi kwa wakati ili wananchi wapate haki zao."

## Serikali yataja utoaji motisha kwa watumishi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imetaja namna inavyoendelea kutoa motisha za kifedha na zisizo za kifedha kwa watumishi wa umma wakiwamo wanaofanya kazi katika mazingira magumu kwa kuboresha viwango vya posho za kufanya kazi baada ya saa ya kazi.

Aidha, kutoa posho za kujikimu wakati wa kusafiri kikazi, miundombinu ya barabara, mawasiliano, kufikisha huduma za umeme kupitia REA, kujenga madarasa na nyumba za walimu zenye staha, kusogeza huduma za kibenki pamoja na mifumo ya huduma za kifedha kuboresha mipango ya motisha na mikataba ya hali bora ya taasisi.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Same Mashariki (CCM), Anne Kilango.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji kuna mkakati gani wa kutoa motisha kwa watumishi wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu.

Akijibu swali hilo, Kikwete alisema pia halmashauri zilizopo katika maeneo yenye mazingira magumu kwa kutambua umuhimu wa kutoa motisha, zinatekeleza mipango yao ya motisha kwa miongozo kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kusimamia utoaji wa motisha mbalimbali kwa watumishi wao kutegemeana na hali ya mazingira magumu yaliyopo katika maeneo husika.

# Gambo ahoji serikali mapitio kikokotoo cha asilimia 33

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, amehoji mpango wa serikali wa kufanya mapitio ya malipo ya mkupuo (kikokotoo) ya asilimia 33 kwa wafanyakazi.

Gambo alisema kanuni mpya ya mafao pensheni imekwenda kupunguza asilimia 50 ya mafao ya mkupuo na kupunguza miaka ya kuishi mtu anapostaafu kazi kutoka 15.5 hadi 12.5 na kuhoji serikali haioni umuhimu wa kurudisha kanuni ya awali.

Akijibu maswali hayo, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema serikali ilitangaza matumizi ya kanuni mpya ya mafao ya pensheni kuanzia Julai Mosi, 2022.

"Kanuni hiyo iliandaliwa kwa kushirikisha

wadau wote (serikali, wafanyakazi na waajiri) kwa lengo la kufanya maboresho ya pensheni ili kuwianisha mafao ya wanachama na kuifanya mifuko kuwa endelevu," alisema.

Alisema kuwa serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mafao ya pensheni ikijumuisha malipo ya mkupuo kwa wafanyakazi.

"Sheria inaitaka mifuko kufanya tathmini ya kupima uhimilivu kila baada ya miaka mitatu na kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali ikijumuisha maboresho ya mafao ya wanachama na kuifanya mifuko kuwa endelevu," alisema.

Alisema kwa kuwa mifuko itafanya tathmini kwa hesabu zinazoishia Juni 2023, serikali itazingatia ushauri wa mtaalam ambaye atafanya tathmini hiyo ili kuongeza pensheni ya wastaafu ambayo inajumuisha malipo ya mkupuo wa asilimia 33.

Aidha, alisema asilimia 81 ya hali ya kikokotoo cha sasa inawapa faida wafanyakazi kwa kuwa na mkupuo mkubwa na asilimia 19 wanabaki na mkupuo wa wastani na mapato ya kila mwezi yameongezeka.

"Serikali chini ya Rais Samia ina nia ya dhati kukitoa kikokotoo hiki kutoka asilimia 25 hadi 33 na tathmini itakayofanyika ikiangalia ustahimilivu wa mfuko itaangalia maslahi ya wafanyakazi na kwenda kutoa faida itakayowasaidia wao ambao wamelitumikia taifa," alisema.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete (kulia), akijadiliana jambo na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mitaa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sh. bilioni 45 kunufaisha wakulima kilimo biashara

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHILINGI bilioni 4.5 zimepangwa kuwafikia wakulima 10,000 kwa ajili ya kuwawezesha kuzalisha mazao mengi katika eneo dogo kupitia mradi wa kilimo biashara.

Mkurugenzi wa Sustainable Environment Management Action (SEMA), Ivo Manyaku, alisema hayo juzi kwenye kikao kazi cha kutathmini utekelezaji wa mradi huo wa miaka mitano ulioanza Septemba 20, 2021 ambao unatarajia kumalizika Juni, 2026.

Utekelezaji wa mradi huo unafanywa kwa kushirikiana na Shirika la Stromme Foundation Tanzania, nchi ya Norway pamoja na wadau wa kimkakati, NGI, CSFS na NMBU.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wa mradi huo wamepata mafanikio makubwa kwa kuongeza uzalishaji wa mazao kwa wakulima kwa kutoa elimu za teknolojia mbalimbali za kilimo.

Manyaku alisema mradi huo ni mahususi kwa vijana na wanawake na ni mwendelezo wa vikundi vilivyokuwa vikitumika katika mradi wa awali wa kuweka na kukopa na wataingizwa katika uzalishaji na kuongeza thamani kupitia mazao ya kilimo ambayo ni mahindi, alizeti, mtama na mbaazi.

Aidha, Manyaku alisema kupitia mradi huo wamefanikiwa kuwatafutia wakulima masoko kwa kuwaunganisha na wadau mbalimbali na wafanyabiashara.

Alisema, lengo la mradi huo ni kuwafikia wakulima 6,000 na kati ya hao asilimia 40 wawe vijana na asilimia mbili watu wenye ulemavu na kuwa umejikita kuhakikisha kuwa teknolojia wanazo wapa zinaendelea kuwasaidia wakulima hata baada ya mradi huo kukamilika.

Alisema pamoja na kuwa na lengo la kuwafikia wakulima 6,000 lakini kwa kupitia mnyororo wa thamani wanatamani kuwafikia wakulima 10,000 katika wilaya ambazo unafanyika mradi huo ambazo ni Iramba, Ikungi na Manyoni zilizopo mkoani Singida.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga, alipongeza mashirika hayo kwa kusaidia Mkoa wa Singida katika sekta ya kilimo.

"Katika mradi huu ni Singida peke yake ndiyo inasaidiwa kuhakikisha inaboresha kilimo ili kuongeza uzalishaji na hasa kwa kutumia teknolojia inayokwenda kuhifadhi maji katika mashamba yetu na kurutubisha ardhi na kuboresha maisha ya familia zetu," alisema.

Alisema pamoja na mambo mengine mradi huo unakwenda kuwawezesha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupata chakula wakiwa shuleni na kutaongeza ufaulu wao.

Wajasiriamali na wanufaika wa mradi huo, Anna Ntandu, kutoka Wilaya ya Ikungi na Rehema Mwaliwa kutoka Kata ya Iseke, wilayani Ikungi waliyashukuru mashirika hayo kwa kuwapa mafunzo ya kilimo biashara ambayo yamewakomboa kiuchumi na kujikimu kimaisha na kusomesha watoto wao.

"Changamoto kubwa tuliyonayo ni vifaa vya kufanyia kazi, mtaji na masoko ya uhakika kwa mfano mimi nalazimika kutumia sufuria kwa ajili ya kuoka mkate badala ya oveni naomba tunapo hitimu mafunzo tuwe tunawezeshwa vifaa hivyo hata kwa kukopeshwa," alisema Mwaliwa.





## DC Ileje aahidi kupata ufumbuzi mgogoro wa ardhi

**Na Nebart Msokwa,** ILEJE

MKUU wa Wilaya ya Ileje mkoani Songwe, Farida Mgomi, ameahidi kuupatia ufumbuzi mgogoro wa ardhi katika vijiji vya Sheyo, Kata ya Ibaba na Itale Kata ya Itale wilayani humo ambao umedumu kwa muda mrefu bila suluhu.

Mgomi alitoa ahadi hiyo wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Sheyo, Kata ya Ibaba, wakati wa ziara yake ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi na moja ya changamoto iliyosomwa na Mtendaji wa kijiji hicho ni mgogoro huo ambao haujawahi kupatiwa suluhu.

Aidha, Mgomi aliagiza Ofisi ya Ardhi inatatua mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu na kuwataka wananchi kuwa na subira wakati wataalamu wanajiandaa kwenda kutafuta suluhu ya kudumu.

"Naiagiza Ofisi ya Ardhi kuhakikisha kufikia Novemba 11, 2023 mfike eneo la mgogoro mkae na pande zote mbili mmalize mgogoro huo ili wananchi waendelee na shughuli zao za kiuchumi bila tatizo," alisema Mgomi.

Kaimu Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Ileje, Yanga Yanga, alisema kufikia Novemba 11, 2023 wanatarajia kukutana na pande zote mbili na wazee maarufu ili kumaliza mgogoro huo na watahakikisha pande zote zinapata haki.

Aliwataka viongozi wa vijiji hivyo pamoja na wa kimila kutoa ushirikiano wakati wa utatuzi wa mgogoro huo ili waumalize mapema na shughuli zingine ziendelee.

**"Naiagiza Ofisi ya Ardhi kuhakikisha kufikia Novemba 11, 2023 mfike eneo la mgogoro mkae na pande zote mbili mmalize mgogoro huo ili wananchi waendelee na shughuli zao za kiuchumi bila tatizo," alisema Mgomi.**

# CCM yaagiza hospitali kutoshikilia miili ya waliofariki wakipatiwa matibabu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mbeya, kimeiagiza serikali mkoani humo kupiga marufuku hospitali zote kushikilia maiti za watu wanaofariki wakati wanapatiwa matibabu kwenye hospitali hizo kwa sababu ya aina yoyote.

Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Christopher Uhagile, aliyasema hayo jana alipokuwa anatoa taarifa ya kikao cha Halmashauri Kuu ya chama hicho mkoa kwa waandishi wa habari baada ya kuhitimishwa kwa kikao hicho.

Alisema matukio hayo yamekuwa yakisababisha wananchi kukosa imani na serikali na kuwataka watumishi wa hospitali na vituo vyote vya kutolea huduma za afya kuwa waadilifu wakati wa kuwahudumia wananchi.

Vilevile, alisema kwenye kikao hicho cha Halmashauri Kuu, chama kinawataka watumishi wa hospitali na vituo vyote vya kutolea huduma za afya kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kuzingatia miongozo mbalimbali inayotolewa na serikali kuu.

"Pia chama kimeielekeza serikali kuagiza hospitali zote ndani ya mkoa kuboresha huduma kwa wananchi hasa kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Serikali Kuu ikiwamo kuwahudumia wazee bila ubaguzi wa aina yoyote," alisema Uhagile. Alisema huduma hizo zinapoboreshwa zinafanya wananchi kuwa na maisha bora na kuiamini serikali yao inayoundwa na chama hicho tawala.

Katika hatua nyingine, Uhagile alisema chama kiliielekeza serikali kuitaka Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), mkoani humo kuharakisha ujenzi wa miundombinu ya barabara kwenye mtandao wao wanapopata fedha ili kuwasogezea wananchi huduma.

Alisema katika Jiji la Mbeya, waliitaka TARURA kukamilisha Barabara ya Vunjabei-Old Airport ambayo imekuwa ikisausa ili kuwarahisishia wananchi usafiri.

Vilevile, alisema chama hicho kiliwaelekeza viongozi wote wa kuchaguliwa na wananchi wakiwamo wabunge na madiwani kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi ili wananchi waendelee kuwa na imani na chama hicho.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kusikiliza kero hizo za wananchi kupitia mikutano ya hadhara ambayo kwa sasa inaruhusiwa kufanyika kwenye maeneo yao.

Hata hivyo, alisema chama hicho kinazitaka idara zote zilizopo ndani ya mkoa huo kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi ili wapate wanazostahili ikiwa ni pamoja na matumizi mazuri ya fedha za umma.



Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Mpunga cha Usangu Farmers Co-operative Society Ltd cha wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, Iddi Mtiginjola, akizungumza na wanachama wakati wa uzinduzi wa bodi mpya ya chama hicho, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mtaka: Hatutawavumilia wazazi wanaoozesha binti zao

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, amesema serikali ya mkoa huo haitawavumilia wazazi na walezi wanaochukua posa na kuwaozesha watoto wao badala ya kuwapeleka shuleni.

Mtaka aliyasema hayo wakati akizungumza na wanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mabatini, Halmashauri ya Mji Njombe kuhusu maandalizi ya mtihani wao wa mwisho.

"Huyu mtoto maskini wa watu anaweza akaamua nini kwenye maisha yake kwamba usinilazimishe mimi mtoto wangu aende shule au asiende, huyu mtoto umri huu anaamua nini, darasa la saba katoto kadogo haka unapokea posa ya kwenda wapi, kwamba umepokea posa ya kwenda wapi hawa watoto, anaenda leba huyu hata kuchumbiwa anachumbiwaje huyu," alihoji Mtaka na kuongeza.

"Ndiyo maana mkiona kwenye taarifa ya Rais, tunamimba nyingi za utotoni kwa maana hawa watoto wanajiandaa kwenda kidato cha kwanza serikali ikisema asilimia 80 ya watoto wa darasa la saba wameenda kidato cha kwanza maana yake asilimia 20 waliobaki nyumbani ni baba na mama ni wazazi," alisema.

Mtaka alisema wazazi wa wanafunzi waliomaliza darasa la saba mwaka huu ambao hawapo tayari kuwapeleka watoto wao shuleni kujiunga na masomo ya sekondari mwakani endapo watafaulu wanatakiwa kuhama Mkoa wa Njombe.

"Kama kuna mzazi ana mtoto nyumbani amemaliza darasa la saba amefaulu kwenda kidato cha kwanza na hana mpango wa kumpeleka ahame huu mkoa watu zamani walikuwa wanakimbia kodi za kichwa wao watakimbia na nyumba," alisema Mtaka.

Alisema serikali imejenga madarasa na kupeleka madawati na vitabu katika shule zote hapa nchini hivyo hakuna sababu ya mzazi kuacha kumpeleka mtoto wake shuleni.

Aliwatakia maandalizi mema wanafunzi wote wa kidato cha nne mkoani Njombe ambao wanatarajia kufanya mtihani wa taifa wa kidato cha nne utakaoanza mwezi Novemba 13, mwaka huu.

Ofisa Elimu Mkoa wa Njombe, Nelasi Mulungu, alisema maandalizi kuelekea mtihani wa taifa kidato cha nne mkoani Njombe yanaendelea vizuri na yalianza tangu wakiwa kidato cha kwanza.

Diwani wa Kata ya Njombe Mjini, Alatanga Nyagawa, alisema elimu kwenye kata hiyo imepewa kipaumbele ili kiwango kipande.





# Kumekucha ZEC uandikishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), inatarajia kuanza uandikishaji wa wapigakura wapya kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Akizungumza jana na wadau wa uchaguzi visiwani hapa, Mwenyekiti wa ZEC, Jaji Joseph Kazi, alisema kazi hiyo itaanza Desemba 2, mwaka huu, na kumaliza Januari 15, mwakani.

Alisema tume hiyo inatarajia kuandikisha wapigakura wapya 162,606 na uandikishaji huo utaanzia wilaya ya Micheweni, Pemba.

Jaji Kazi alisema kila wilaya uandikishaji utadumu kwa siku tatu na mwananchi ambaye ana sifa na hajapata fursa ndani ya siku hizo tatu, uandikishaji utaendelea katika ofisi za tume ya uchaguzi ili kila mmoja kupata haki hiyo.

Alisema uandikishaji huo ni kwa wale wenye sifa ambao hawamo katika daftari la wapigakura lililoandaliwa mwaka 2020.

Mwenyekiti huyo alizitaja baadhi ya sifa hizo ni kufikisha umri wa miaka 18 na kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Jaji Kazi aliwataka wananchi kudumisha amani katika kipindi chote cha uandikishaji na baada ya hapo, wale wote wenye sifa kujitokeza katika kujiandikisha.

Akiwasilisha mada kuhusu taarifa na utaratibu wa uandikishwaji wa wapigakura na uendeshaji wa daftari la kudumu la wapigakura, Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Idarous Faina, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 2018, ZEC imepewa jukumu la kuandaa, kutayarisha, kuhifadhi na kuendeleza daftari la kudumu la wapigakura.

Alisema kwa Wilaya ya Micheweni Pemba ambako uandikishaji utaanzia, wananchi 10,907 wanatarajiwa kuandikishwa, Wilaya ya Wete 12,705, Chakechake 11,682 na Mkoani 11,964.

Kwa wilaya za Unguja, alisema Kaskazini A inatarajiwa kuandikisha watu 7,880, Kaskazini B 13,169, Wilaya ya Kati 10,438, Kusini 4,792, Magharibi 'A' 28,677, Magharibi B 31,120 na Mjini 19,272.

Pia alisema endapo mwombaji atakuwa hakuridhika na uamuzi wa mkuu wa kituo, atawasilisha pingamizi kwa ofisa uandikishaji wa wilaya juu ya uamuzi huo na ofisa uandikishaji wa wilaya atasikiliza pingamizi hilo.

"Endapo mwombaji hakuridhika na uamuzi wa afisa uandikishaji anaweza ndani ya kipindi cha siku saba, kuanzia tarehe ya uamuzi huo, kuwasilisha rufani Tume ya Uchaguzi," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa ZEC, Maulid Ame Mohamed, akiwasilisha mada nafasi ya sheria ya uchaguzi katika uandikishaji na uendeshaji wa daftari la kudumu la wapigakura, alisema iwapo mtu atafanya moja ya makosa yaliyoainishwa ikiwamo kutoa taarifa za uongo, atalipa faini isiyozidi Sh. milioni tatu na isiyopungua Sh. 300,000.

Alisema au atatumikia kifungo jela kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita.

Pia alisema sheria ya uchaguzi imeweka utaratibu mzuri wa kujiandikisha kwa mtu mwenye sifa, hivyo aliwataka wadau wa uchaguzi kuisoma na kuielewa sheria hiyo na kanuni zake ili kushiriki katika uandikishwaji bila matatizo.

## Manispaa Magharibi B yakusanya mil. 470.7/-

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BARAZA la Manispaa Magharibi B Unguja, limekusanya Sh. 470,673,890 kwa kipindi cha robo ya kwanza, kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Mkurugenzi wa Baraza hilo, Khadija Said Simai, aliyasema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa ofisi kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, katika kikao cha Baraza la Madiwani, Momba kwa Mchina Unguja.

Alisema fedha hizo ni kutoka vyanzo vya ndani vya mapato pamoja na ukaguzi wa leseni, maghala, viwanda, gereji, maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Pia alisema fedha hizo ni sawa na asilimia 72 ya makusanyo ya robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Mkurugenzi huyo alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kutimiza miaka mitatu ya uongozi na kuleta maendeleo katika sekta mbalimbali.

Alisema baraza limekadiria kukusanya Sh. milioni 651,420,000 kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, ingawa hazikufika kutokana na kukosa mapato kwa baadhi ya vyanzo.

Kuhusu uimarishaji mji, alisema baraza limezoa taka tani 3,423 taka ngumu na kupelekwa jalala kubwa Kibele.

Naye Mstahiki Meya Baraza la Manispaa Magharibi B, Khamiss Hassan Haji, aliwataka wajumbe wa kikao hicho kushirikiana na watendaji wa baraza hilo ili kufikia malengo yaliyotarajiwa.

Wajumbe wa baraza hilo, walisema wataendelea kushirikiana na watendaji ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato sambamba na kupita kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kuhamasisha kulipa kodi.



Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Uwekezaji (TIC), Dk. Binilith Mahenge (kulia), akiangalia nyaya zinazotengenezwa na kiwanda cha Akberalis Hardware and Electric Ltd cha jijini Dar es Salaam alipotembelea jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Hussein Alibhai. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Taasisi yajitosa kuimarisha mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuunga mkono juhudi za maendeleo ya Zanzibar, Taasisi ya Maendeleo Zanzibar (TAZAMA) inakusudia kuimarisha mazingira bora visiwani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa TAMAZA, Makame Handhar Khamis, alisema suala la mazingira ni mtambuka na ni muhimu kwa sababu limebeba maisha ya watu na bila mazingira bora, maisha ya watu yatakabiliwa na majanga mbalimbali yatokanayo na athari za kimazingira.

Alisema changamoto za kimazingira yakiwamo mabadiliko ya tabianchi, mabadiliko ya ekolojia na mengineyo ambayo yamefanywa na mwanadamu duniani kote hasa katika karne hii ya sayansi na teknolojia, yameathiri sana maisha ya mwanadamu.

Mabadiliko hayo, alisema yamesababisha madhara makubwa yakiwamo kuongezeka kwa hali ya joto, kukauka kwa vyanzo vya maji, misitu kugeuka majangwa na binadamu kuleta hali ya ukaa.

"Mambo hayo yameikumba dunia na Zanzibar kwa upana na urefu wa matatizo hayo. Na sisi vijana tulioshinda uzalendo tumejikusanya na kuunda asasi hii ili kusaidia juhudi za kupambana na changamoto za kimazingira," alisema.

Alisema miongoni mwa malengo makuu matatu ya taasisi hiyo ni kurejesha Zanzibar ya kijani, kuelezea fursa zilizoko katika sekta ya uchumi wa buluu na kuunga mkono juhudi za maendeleo ya Zanzibar.

Pia alisema hivi sasa Zanzibar inafanya mapinduzi makubwa ya kimiundombinu ambayo baadhi ya miti imekatwa ili kupisha ujenzi huo.

Naye Katibu wa TAZAMA, Iddi Thabit, alisema kuwa uwepo wa taasisi hiyo kutasaidia pia kuhamasisha maendeleo ya jamii hasa katika kujengewa uwezo juu ya masuala yanayowagusa.

Taasisi hiyo inatarajiwa kuzinduliwa Novemba 11, mwaka huu na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**PENDO AMOS NDAHYA** anatangaza kupotelewa na vyeti, cheti cha kuhutimu kidato cha nne cheye index No. P0605-0098 Kilichotolewa na **UHURU SECONDARY SCHOOL CENTRE** mwaka 2017, cheti cha chuo **ORDINARY DIPLOMA IN CLINICAL MEDICINE No. NP0605/0098/2017** kilichotolewa na **KOLANDOTO COLLEGE OF HEALTH SCIENCES** mwaka 2021 pamoja na **ACADEMIC TRANSCRIPT**. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: KRU/RB/1416/2022.**

## KUPOTEA KWA OFFER YA KIWANJA

**SALUM JUMA NASORO** anatangaza kupotea kwa offer ya umiliki wa kiwanja **PLOT NO. 50, BLOCK D, ILAZO WEST-DODOMA CITY COUNCIL.** Yeyote atakayeiyona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**PHQ/DOD/DOD/8056/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PEACE GODWIN MASASI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina ISMAIL RAMADHANI MALENDA namba za usajili T784ECC aina ya TOYOTA LITEICE, Chassis No. KM700007200. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:

**PHQ/DOD/DOD/8125/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MENRAD HUBERT RWABUTAZA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA PREMIO** yenye jina la umiliki **SOFTECH CONSULTANTS LTD.** usajili namba **T 108 BKT, CHASSIS NAMBA: ZZT2400008740 na ENGINE NAMBA: 1ZZ0949865.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/31151/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NISHIT VIRENDRA VORA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA CRESTA** yenye usajili **T 679 ARG.** Chassis namba: **GX1006058629** Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha karibu.

Taarifa Polisi:

**PHQ/TAN/2414/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JACOB WILFRED KIBONA** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE326251** iliyotolewa uhamiaji makao makuu **DAR ES SALAAM** mnamo tarehe **23/03/2020.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIG/97351/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DALGHA MAKSUD SHINGANYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T806DRZ aina ya Suzuki Escudo, Chassis namba **TD52W103004** na Engine namba **J20A118444.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

TAARIFA YA POLISI

**PHQ/MAN/ BAB/1848/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER CHACHA MGINE** anatangaza kupotelewa na Kadi ya gari yenye namba za usajili T.528 DMA aina ya TOYOTA SUCCEED. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **TAR/RB/1082/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA. 18/2023**
**SIMON CHIWANGA ............MWOMBAJI**
**NA**
**PASACAL M. KAGUSA & 36 OTHERS............WAJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**17. SIMON MATUMBI, 18. GISION STEPHANO TOGWA, 19. PATRICK WOISO, 20. MRISHO MAILIKI MRISHO, 21. SHIDA MARIO MWITA, 22. AMOS ZEBEDAYO NOAH, 23. MLEWA, 24. CARLOS, 25. JULIUS, 26. SHAYO, 27. PIUS, 28. ASHA, 29. JACOB ELIZABERT, 30. KATARINA MATHI, 31. MOHAMED WILLIUM, 32. MWALIMU SAID OMARY, 33. MRISHO, 34. IDDY MARIA, 35. MOHAMED HATH, 36. DEO MBOYA, 37. SEVERIN MZORA**

**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA RUFAA YA ARDHI NA. 18/2023 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA:** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama kuu ya Tanzania, Kanda ya Dodoma, Mbele ya Jaji,S. H. Hassan, wa Mahakama kuu Dodoma, saa tatu (3:00) asubuhi siku ya Jumatatu tarehe 13/11/2023.

HIVYO BASI unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

NA ENDAPO; hutafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

IMETOLEWA; kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo 22 mwezi wa Septemba, 2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA. 18/2023**
**SIMON CHIWANGA ........MWOMBAJI**
**NA**
**PASACAL M. KAGUSA & 36 OTHERS.........WAJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**1.PASACAL KAGUKAGUSA, 2. ALLY A. SACOKA, 3. EMMY MBONDE, 4. DAVID MSAHALA MABWAI, 5. RABIA ALLY, 6. AUGUSTINO, 7. KARINA MATHIAS, 8. JACON ELIZABERTH, 9. GRADINO COSMAS, 10. HOSEA MWANTEU, 11. DEO MBOYA, 12. ISMAIL 13. DANIEL MWANI TEVU, 14. MATHA JOHN RAJAB, 15. STEPHANO MICHAEL, 16. ANTONI CLAUDIA MDOMA,**

**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA RUFAA YA ARDHI NA. 18/2023**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA:** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama kuu ya Tanzania, Kanda ya Dodoma, Mbele ya Jaji,S. H. Hassan, wa Mahakama kuu Dodoma, saa tatu (3:00) asubuhi siku ya Jumatatu tarehe 13/11/2023.

HIVYO BASI unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

NA ENDAPO; hutafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

IMETOLEWA; kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo 22 mwezi wa Septemba, 2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

## KUPOTEA KWA CHETI



**MUNETE FRANCIS BURIRO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba P0806/0280 kilichotolewa na CITY SEC SCHOOL CENTRE mwaka 2006. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: PHQ/DOD/DOD/7438/2023.**

## KUFUNGA KAMPUNI

**HAMTZA LIMITED NAMBA YA USAJILI 152965834** Inapenda kuwatangazia rasmi wadau wake kupitia maamuzi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya **HAMTZA LIMITED INAFUNGWA RASMI.** Hivyo mwenye madai yeyote afike Ofisini kuwasilisha madai yake.

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI......498 LA 2023**
**OTHMAN RAMADHANI SIMBA........................MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **NATIONAL BANK OF COMMERCE LIMITED**
- **ISHENGOMA KARUME MWASHA & MAGAI......MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

- **NATIONAL BANK OF COMMERCE LIMITED**
- **ISHENGOMA KARUME MWASHA & MAGAI**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**OTHMAN RAMADHANI SIMBA** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 5/12/2023 saa 3:00 Asubuhi mbele ya J.W SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 08 Mwezi 11, 2023

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.117 OF 2023**
**IN the Matter of the late:**
**LUCIAN FABIAN MAARIFA**

**By 1.LAUTELI ELIAS MAARIFA**
**2.........................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 27 day of November 2023.

Dated at Morogoro this 02 day of November 2023.

**RESIDENT MAGISTRATE**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.116 OF 2023**
**IN the Matter of the late:**
**KATARINA KOBELSKI JAMBIYA**

**By 1.KASSIM RAMADHANI KOPA**
**2.........................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 27 day of November 2023.

Dated at Morogoro this 02 day of November 2023.

**RESIDENT MAGISTRATE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA LILILOPO BUKOBA KAGERA.**
**MAOMBI NA. 07/2023**
**DR. PROJESTUS KWEYAMBA ..................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **GLORIA FRANCIS**
- **MEDARD DAUD MWIJAGE............WAJIBU MAOMBI**

**KWA: GLORIA FRANCIS NA MEDARD DAUD MWIJAGE**

**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa kuwa Maombi Na. 07/2023 yamepangwa kujatwa tarehe 15/11/2023 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, P. J. Makwandi saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria ninyi wenyewe / mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 11/10/2023.

.......................................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA - BUKOBA**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0745 700 710.*

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.141 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late of the late**
**WILSON MAGOBO SAJILO**
**AND**
**In the matter of application for letters of administration by LAZARO WILSON MWALUKO**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner thereof.

Objections to the grant should be filed on or before the 29 Day of 11, 2023

Dated at Dodoma this 08 day of 11, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Wanajeshi wa Israel wakiwa na mbwa katika doria, huko ukanda wa Gaza, jana. **PICHA: MTANDAO**

# G7 yaiunga mkono Israel

- Yasema Israel inahaki ya kujilinda
- Yashinikiza uharaka kuwasaidia raia

**Na Maulid Mmbaga**

MAWAZIRI wa Mambo ya Nje wa Mataifa saba yanayoongoza kwa uchumi wa viwanda (G7) wamelaani kundi la wapiganaji wa Hamas na kuunga mkono haki ya Israel ya kujilinda, licha ya kushinikiza hatua za haraka za usitishwaji wa vita ili kupisha misaada ya kibinadamu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na G7 jana, wanadiplomasia hao baada ya kukutana mjini Tokyo nchini Japan, mkutano huo unakusudia kusawazisha ukosoaji wa mashambulizi ya Hamas na uungaji mkono kwa Israel, licha ya kueleza kwamba raia huko Palestina wanahitaji sana chakula, maji, huduma za matibabu na makazi.

Inaelezwa kuwa mawaziri hao kutoka Marekani, Uingereza, Kanada, Ufaransa, Ujerumani, Japan na Italia, wanasisitiza kwamba wanaunga mkono usitishaji wa vita kwa ajili ya misaada ya kibinadamu ili kuwezesha usaidizi unaohitajika haraka, harakati za kiraia na kuachiliwa kwa mateka.

Inabainishwa kuwa katika mazungumzo yao kulikuwa pia na kulaaniwa kwa kuongezeka kwa ghasia za walowezi wenye itikadi kali zinazofanywa dhidi ya Wapalestina, wakisema “haikubaliki, inadhoofisha usalama katika Ukingo wa Magharibi na inatishia matarajio ya amani ya kudumu”.

**HALI YA VIFO**

Kwa mujibu wa Jumuiya ya Wafungwa wa Palestina, takriban Wapalestina 154 wameuawa na 2,150 kukamatwa na vikosi vya Israel katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu tangu vita vya Israel na Hamas vilipozuka mwezi Oktoba.

Inaelezwa kuwa tangu Oktoba 7, mwaka huu, mashambulizi ya Israel yameua zaidi ya Wapalestina 10,000, karibu asilimia 40 kati yao wakiwa watoto, kulingana na hesabu za maofisa wa afya wa Gaza.

Aidha, wanadiplomasia hao walipokutana, Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) lilisema maelfu ya Wapalestina huko Gaza wanakimbia kwa miguu kuelekea kusini, huku wakibeba tu kile wanachoweza baada ya kukosa chakula na maji kaskazini.

> “Kiongozi wa cheo cha juu wa Hamas, Yahya Sinwar, ametengwa kwenye handaki lake huku wanajeshi wa Israel wakiendelea kukaza kamba kuuzunguka mji wa Gaza.

Kwa mujibu wa takwimu za UN, takriban theluthi mbili ya wakazi milioni 2.3 wa Gaza ni wakimbizi wa ndani, huku maelfu wakitafuta hifadhi katika hospitali, ikiwa ni pamoja na katika makazi ya muda ya turubai katika maeneo ya kuegesha magari.

Pia inaelezwa kuwa hospitali katika eneo lote la Gaza zimekabiliwa na moto, huku wengi wakijitahidi kuendelea kufanya kazi huku kukiwa na uhaba wa mafuta na vifaa vya matibabu.

UN inasema huduma za afya, usafi wa mazingira, maji na chakula za Gaza zinakaribia kuvunjika.

**GAZA YAZINGIRWA**

Waziri wa ulinzi wa Israel, Yoav Gallant, anasema wanajeshi wa Israel wanaendesha harakati katikati mwa Gaza yenye idadi kubwa ya watu.

Anabainisha kuwa wanajeshi wake walikuwa wakipambana na wapiganaji wa Hamas ndani kabisa ya mji wa Gaza, ambayo ilikuwa na watu takribani 650,000 kabla ya vita, huku Jeshi likisema Hamas ina amri yake kuu na labyrinth kubwa ya vichuguu.

Anasema kiongozi wa cheo cha juu wa Hamas, Yahya Sinwar, ametengwa kwenye handaki lake huku wanajeshi wa Israel wakiendelea kukaza kamba kuuzunguka mji wa Gaza.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, anasema Israel itafikiria sitisho la muda mfupi la mapigano katika operesheni zake za kijeshi ili kuruhusu misaada ya kibinadamu kufika huko Ukanda wa Gaza au kwa mateka wanaoshikiliwa na Hamas kuondoka huko.

Licha ya kauli hiyo, ila inaelezwa kuwa alifuta uwezekano wa sitisho la jumla la mapigano katika vita vilivyodumu kwa mwezi mmoja sasa.

Akizungumza na kituo cha televisheni cha ABC News, Netanyahu anasema anatarajia Israel itakuwa na jukumu la jumla la usalama huko Gaza kwa muda usiojulikana baada ya kufikia lengo lake la kuwaondoa Hamas.

“Wakati hatuna jukumu la usalama, kile tulichonacho ni kuibuka kwa ugaidi wa Hamas kwa kiwango ambacho hatuwezi kukifikiria,” amesema Netanyahu.

**UNRWA**

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia utoaji wa misaada ya kibinadamu katika ardhi ya Wapalestina, (UNRWA) linasema jumla ya maofisa wake 89 wameuawa na wengine karibu 26 kujeruhiwa tangu vita hivyo vianze, ikieleza kuwa hiyo ndiyo idadi kubwa ya wafanyakazi wa UN kuuliwa katika historia ya umoja huo.

Wiki hii shirika hilo lilisema takriban watu milioni 1.5 wamelazimika kuyahama makazi yao huko Gaza kutokana na vita hivyo, ikiwa ni sawa na takriban asilimia 70 ya idadi jumla ya wakazi.

Inabainisha kuwa karibu nusu ya wakazi hao walikuwa wamepewa hifadhi na wanaishi katika maeneo ya Shirika la UNRWA, ikiwamo kwenye shule.

Taarifa ya shirika hilo inasema karibu vituo 50 vimeathiriwa tangu mzozo ulipozuka na mtu mmoja aliyekuwa ameyahama makazi yake aliuliwa na wengine tisa kujeruhiwa katika kituo kimoja kaskazini mwa ukanda wa Gaza baada ya kulengwa moja moja na mashambulizi.

**AHADI YA MAREKANI**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, anasema kwamba, atafanya kazi ili kuzuwia kuenea kwa mzozo wa Hamas na Israel baada ya waasi hao wa Yemen na wale wa Lebanon wa Hezbollah kurusha makombora nchini Israel.

Vile vile, mataifa mengi katika kanda ya Mashariki ya Kati yamekosoa namna Israel inavyoendelea kuishambulia Gaza, hasa baada ya hospitali moja kulengwa ambayo kwa mujibu wa Hamas shambulio hilo liliwaua mamia ya watu, huku Israel ikikanusha kuhusika nalo.

Naye mshauri wa Rais wa Marekani Joe Biden, Amos Hochstein, amefanya ziara ambayo haikutangazwa mjini Beirut kwa ajili ya mazungumzo na spika wa bunge la Lebanon na waziri mkuu wa mpito na kwamba katika mazungumzo hayo amesisitiza kuwa kurejeshwa kwa utulivu katika mpaka wa kusini wa Lebanon ni suala la umuhimu mkubwa.

Anasema Marekani haitaki kuona mzozo wa Gaza unaendelea na kutanuka hadi Lebanon.

**WANAHABARI 41 WAUAWA**

Katika hatua nyingine Shirika la Waandishi Habari Wasio na Mipaka, (RSF), linasema limerekodi vifo 41 vya waandishi wa habari tangu kuanza kwa vita kati ya Hamas na Israel, na kwamba miongoni mwao walikutwa na umauti wakati wakitekeleza majukumu yao.

Shirika hilo limetoa wito kwa waandishi wote huko Gaza walindwe na waandishi wa kigeni waruhusiwe kuingia na kufanya kazi kwa uhuru.

Ripoti ya shirika hilo inasema katika idadi hiyo mmoja aliuliwa nchini Lebanon siku za mwanzo za vita vya Gaza na wengine wanne wa Israel waliuliwa katika shambulizi la Hamas Oktoba 7.

***Chanzo mashirika ya kimataifa***

HABARI MICHEZO

# MAXI AWATAKA NYOTA YANGA KUTOBWETEKA

**Na Faustine Feliciane**

WINGA wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Maxi Nzengeli, amewataka wachezaji wenzake katika timu hiyo kusahau ushindi mnono wa mabao 5-1 walioupata dhidi ya watani zao Simba na badala yake waelekeze akili na nguvu kwenye michezo inayofuata.

Maxi aliliambia gazeti hili kuifunga Simba sio mwisho wa ligi kwani bado wana michezo mingi mbele yao ambayo wanatakiwa kufanya vizuri ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kutetea ubingwa wao.

"Bado tuna michezo mingi mbele yetu, ni kweli tunafuraha sana kupata ushindi mzuri dhidi ya Simba, lakini mapambano bado yanaendelea, tunatakiwa sasa kuelekeza akili na nguvu katika michezo inayofuata, hatutakiwi kubweteka," alisema winga huyo.

**Aliongeza ushindi dhidi ya Simba unapaswa kuwaongezea morali na hali ya kupambana kuelekea michezo inayofuata ya ligi hiyo yenye timu 16.**

"Kuwafunga wapinzani wako wakubwa katika mbio za ubingwa kunakuongezea hali ya kujiamini na kupambana zaidi, tulipata ushindi dhidi ya Azam na sasa dhidi ya Simba, hii kwetu itaongeze morali kwetu wachezaji," alisema nyota huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Maxi alifunga mabao mawili huku mengine yakifungwa na Kennedy Musonda, Stephanie Aziz Ki na Pacome Zouzoua.

Kabla ya mechi ya jana jioni, Yanga iliyokuwa na pointi 21, iko kileleni ikifuatiwa na Azam FC yenye pointi 19 na Simba yenye pointi 18 iko katika nafasi ya tatu huku Mtibwa Sugar yenye pointi tano inaburuza mkia.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa Simba kuikaribisha Namungo kutoka Lindi kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, mechi ya kukamilisha raundi ya tisa.



# Tanzanite yaipigia hesabu Nigeria

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20, (Tanzanite) kinaendelea vyema na mazoezi yake kwa ajili ya kujiandaa kuwakaribisha wapinzani wao, Nigeria katika mchezo wa kwanza wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo alisema timu hiyo imeshaingia kambini na wanaamini wachezaji wake watapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri hapa nyumbani ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele.

Ndimbo alisema wanafahamu hakuna mechi rahisi kwa sababu wanaamini wapinzani wao watakuja nchini na lengo moja la kusaka ushindi.

"Timu iko kambini na kuendelea na mazoezi kwenye Uwanja wa Uhuru ili kuwakabili Nigeria, kikosi kiko tayari kwa ajili ya mchezo huo ambao tutaanzia nyumbani, kila kitu kinakwenda vyema," alisema Ndimbo.

Naye Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, alisema maandalizi yanaenda vizuri na anachokifanya ni kuwaandaa wachezaji wake kimbinu na ufundi.

"Tunaendelea na maandalizi yetu na vijana wako vizuri, kwa sasa tunaangalia zaidi mbinu na ufundi baada ya hapo tunaenda kufanyia kazi ubora na madhaifu ya wapinzani wetu," alisema Shime.



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), Zainab Mohamed (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa timu hiyo katika mazoezi ya kuikaribisha Nigeria kwenye mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia U-20 itakayochezwa Jumapili. **PICHA: TFF**

# Mafunzo, New City hakuna mbabe Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAAFANDE wa Mafunzo wameendelea kusuasua katika Ligi Kuu Zanzibar baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya New City FC katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi jioni.

Hiyo inakuwa sare ya nne kwa Mafunzo, imeshinda mechi moja na imepoteza michezo minne wakati New City yenyewe imeshinda mchezo mmoja, sare tatu na imefungwa michezo mitano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mafunzo, Abdallah Bakari "Edo", alisema licha ya kukiongeza nguvu kikosi chake kwa kutumia wachezaji kutoka timu B, lakini bado wanashindwa kupata matokeo mazuri.

Edo alisema hawezi kuwatupia lawama yoyote wachezaji wake na anaahidi ataendelea kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya kupata matokeo mazuri kwenye mechi zinazofuata.

Kocha huyo alisema mipango na malengo yake yanaharibika kwa sasa kutokana na kupata majeruhi wengi kuanzia mwanzo wa msimu.

"Bado timu yangu inashidam haina muunganiko mzuri baada ya kukibomoa kikosi kwa sababu ya majeruhi, wachezaji niliowapandisha kutoka timu ndogo wanahitaji muda ili kuzoea mbinu za Ligi Kuu, lakini ninashukuru haturusu kufungwa mabao mengi," alisema Edo.

Naye Kocha Msaidizi wa New City, Razak Rajabu, alisema tatizo kubwa linaloitesa timu yake ni kutokuwa na washambuliaji makini.

Rajabu alisema asilimia kubwa ya wachezaji wake wanashindwa kumiliki vyema mpira na wanapoteza umakini wa kufunga pale wanapokaribia lango la wapinzani wao.

"Tunatengeneza nafasi nyingi sana lakini nafasi hizo tunashindwa kuzitumia, mipira yetu tunacheza sana miguuni lakini haifiki mbele tunaposhambulia, hili ndio tatizo linalohitaji kufanyiwa kazi," kocha huyo aliongeza.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Mafunzo yenye pointi saba iko kwenye nafasi ya 13 wakati New City yenye pointi sita ipo nafasi ya pili kutoka mkiani katika ligi hiyo yenye timu 16.

**Katika msimamo wa ligi hiyo, Mafunzo yenye pointi saba iko kwenye nafasi ya 13 wakati New City yenye pointi sita ipo nafasi ya pili kutoka mkiani katika ligi hiyo yenye timu 16.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ODIBO ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United imeonyesha nia ya kumsajili beki wa kati wa Nice, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 23 kama mbadala wa mchezaji, Raphael Varane (30), ambaye anaweza kuelekea Saudi Arabia. ***(caught offside)***

### KELLY AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Bournemouth itakataa mbinu zozote za kumuuza mlinzi, Lloyd Kelly ifikapo Januari, huku Tottenham, Liverpool, Newcastle United na AC Milan zikionyesha nia ya kumnunua Mwingereza huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Teamtalk)***

### 'ANTONY HATAREJEA'

WAKALA wa mlinzi wa Manchester United Mbrazil Antony mwenye miaka 23, amesema mteja wake hatarejea katika nchi yake kwa makubaliano ya kubadilishana mshambuliaji, Gabriel Barbosa (27), ambaye anaichezea Flamengo. ***(Jorge Nicola, via Express)***

### JUVE WAMTAKA PHILLIPS

MIAMBA ya Italia, Juventus inavutiwa na mkataba wa mkopo wa kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27, ambaye anaelekea kuondoka Manchester City katika dirisha la Januari. ***(Team talk)***

### ALCANTARA ATAKILA ITALIA

KIUNGO wa kati wa Liverpool, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 32, analengwa na klabu za Serie A, Juventus na Inter Milan, huku mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania na Wekundu hao ukimalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Fichajes)***

### LOCATELLI KUZEEKEA JUVE

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Italia, Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 25 anatazamiwa kusaini mkataba mpya na Juventus ambayo utamalizika ifikapo Juni, mwaka 2028. ***(Fabrizio Romano)***

### CHELSEA, LIVERPOOL VITANI

CHELSEA na Liverpool zimeweka wazi nia ya kumsajili mlinzi wa Real Betis ya Hispania mwenye umri wa miaka 18, Assane Diao, 18. ***(Mucho Deporte, via Football Talk)***

### DUMFRIES ANUKIA EPL

KLABU za Chelsea na Manchester United zitalazimika kutoa Euro milioni 50 kama wanataka kumsajili beki wa kulia wa Uholanzi, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 27 kutoka Inter Milan ya Italia. ***(CalcioMercato)***


### ANDRE KUTUA ARSENAL

ARSENAL, Fulham na Liverpool zilituma wawakilishi kumtazama kiungo wa Fluminense, Andre wakati wa fainali ya Copa Libertadores. Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 22 ana makubaliano ya kuondoka Januari wa mabingwa hao wa Amerika Kusini, ambapo thamani yake ni euro milioni 35. ***(Globo Esporte)***

### ALONSO KUONDOKA BARCA

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Hispania, Marco Alonso, 32, anatarajiwa kuondoka Barcelona na kujiunga na wapinzani wao wa LaLiga, Atletico Madrid. ***(Football Transfers)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CASEMIRO KURUDI DIMBANI KRISMASI

### Ni baada ya jeraha la kiungo huyo wa kati kubainika ni...

**MANCHESTER,** England

CASEMIRO ameongeza tatizo la majeruhi la Manchester United baada ya Kocha Erik ten Hag kusema kiungo huyo wa kati wa Brazil atakuwa nje ya uwanja hadi Krismasi kutokana na jeraha la misuli ya paja.

**United walikuwa wakingoja kutathmini kiwango kamili cha jeraha alilopata mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 wakati wa kufungwa katika mechi ya Kombe la Carabao dhidi ya Newcastle United iliyochezwa Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Old Trafford.**

Akizungumza nchini Denmark kabla ya mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Ulaya jana dhidi ya FC Copenhagen, Ten Hag alisema Casemiro sasa ataungana na mchezaji mwenzake wa muda mrefu Lisandro Martínez kwenye chumba cha matibabu.

"Natarajia baadhi ya wachezaji waliokuwa majeruhi kurejea, lakini Casemiro na Martinez, ni majeruhi wa nguvu sana na sitarajii kurejea kabla ya Krismasi," alisema Ten Hag. "Ni wiki kadhaa kwa Casemiro."

Casemiro alitolewa wakati wa mapumziko katika mechi ambayo United ilipokea kichapo kutoka kwa Newcastle.

Mabeki wa kushoto Luke Shaw na Tyrell Malacia wote wamekuwa nje ya uwanja tangu wiki za mwanzoni mwa msimu na bado hawajapatikana, huku kiungo wa kati, Kobbie Mainoo akikosa safari ya Copenhagen kutokana na jeraha.

Hata hivyo, Ten Hag alisema Harry Maguire na Marcus Rashford wako fiti kukabiliana na mabingwa hao wa Denmark.

Maguire alicheza dakika zote 90 za ushindi wa Jumamosi dhidi ya Fulham licha ya kwenda chini mara mbili kwa matibabu kutokana na kizunguzungu, wakati Rashford alikosa mchezo baada ya kufeli mtihani wa ufiti kabla ya mechi.

"Tulifanya itifaki zote wakati na baada ya mchezo, kwa hiyo yeye (Maguire) yuko tayari kucheza," kocha huyo raia wa Uholanzi alisema.

## HABARI MICHEZO

# HAALAND AMSHANGAZA GUARDIOLA




**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amekiri, Erling Haaland anaendelea kumshangaza baada ya mshambuliaji huyo wa Manchester City kuonyesha kiwango cha kuvutia zaidi katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Young Boys uliochezwa juzi usiku.

Licha ya kufunga bao lake la 66 na 67 katika mechi yake ya 70 kwa timu hiyo, Guardiola alisema bado anashangazwa na kipaji alichonacho wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0.

Bosi huyo alisema: "Ndiyo bado ananishangaza, kwa sababu kawaida hufunga mabao katika eneo la yadi sita, ya nane na kwa penalti. Lakini ana kipaji hiki, si mara ya kwanza kufanya hivyo.

"Nadhani pasi ya Rico Lewis ilikuwa ya kushangaza. Ninapenda anaposhambulia katika nafasi ya tatu ya mwisho. Mwendo kutoka kwa mpinzani, udhibiti na ana bao hapa.

"Ana bao katika nafasi hiyo wakati hafikirii sana na upigaji wake ni wa ajabu. Ndio, lilikuwa bao la ajabu.

"Bao la Phil Foden pia lilikuwa la kushangaza."

Ushindi huo mzuri kwenye Uwanja wa Etihad uliwafanya vijana wa Guardiola wasonge mbele na kutinga hatua ya mtoano huku kukiwa na michezo miwili imebakia.

Na ingawa City wameifanya ionekane rahisi katika Kundi G hadi sasa, Guardiola alisisitiza hiyo ilikuwa mbali na kesi hiyo.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 52 aliongeza: "Ndio, wakati mwingine unapaswa kupigana dhidi ya tabia ya watu na kile wanachofikiri kuhusu kile kitakachotokea.

"Watu wangesema tutafuzu kwa uhakika na tayari tumefuzu.

"Bado kazi haijakamilika kwa sababu ni lazima tumalize wa kwanza, ni bora mechi ya pili tufuate hatua ya 16 nyumbani kwa sababu tukiwa nyumbani tunajiamini.

"Ni kweli, inavutia sana. Tulifunga mabao mawili ya ajabu. La pili na la tatu ni mabao ya ajabu."

# Xavi: Barcelona tuna hali mbaya

**HAMBURG,** Ujerumani



XAVI Hernández amesema Barcelona wako katika hali mbaya na wanahitaji kujirekebisha baada ya kupokea kichapo cha kushangaza cha bao 1-0 kutoka kwa Shakhtar Donetsk katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya huko iliyochezwa Hamburg, juzi

Danylo Sikan alifunga bao pekee katika mchezo huo muda mfupi kabla ya kipindi cha mapumziko huku Barca wakikosa nafasi ya kujikatia tiketi ya kutinga hatua ya 16 bora.

Mabingwa hao wa Hispania walitawala mchezo, lakini walipiga shuti moja lililolenga lango licha ya kuwaingiza Pedri, Lamine Yamal na João Félix katika kipindi cha pili.

"Tulistahili kupoteza," Xavi alisema katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo huo. "Lazima tuwe wakweli. Tulicheza vibaya na hakuna tulichokuwa tumepanga kikafanikiwa.

"Kiwango cha uchezaji wetu kiko chini sana kwa sasa. Huu ulikuwa ni mchezo mbaya zaidi katika miaka miwili niliyoiongoza. Tunapaswa kujikosoa.

"Kulikuwa na hisia katika kipindi cha pili lakini haikutosha. Mashindano haya yanadai ubora wako na hatukuwa hivyo leo (juzi).

"Tuna hasira. Kujiamini kumeshuka, tuko katika hali mbaya na tunahitaji kurekebishwa.

Barca ilishinda bao 1-0 dhidi ya Real Sociedad mwishoni mwa wiki kwenye LaLiga, lakini Xavi alisema haukubaliki na kukosoa kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake.

Dhidi ya Shakhtar, ambao wamehamishwa kwenda Hamburg kwa mechi za Ulaya kutokana na vita huko Ukraine, kocha wa Barca alisikitishwa zaidi na jinsi walivyocheza.

"Singesema ilikuwa shida kubwa wakati huu," aliongeza. "Hatukuelewa mchezo unahitaji nini.

Tulipoteza mipira mingi, hatukushambulia vizuri, hatukushughulikia vyema krosi na tulilipa makosa yetu."

Barca wanasalia kileleni katika Kundi G wakiwa na pointi tisa kutokana na michezo minne, sawa na FC Porto, huku Shakhtar wakiwa na pointi sita na Royal Antwerp wakiburuza mkia bila pointi mkononi.

"Ni aibu kwa sababu tulitaka kujiandikisha katika hatua ya 16 bora," Xavi alisema.

"Bado tuna sifa katika mikono yetu wenyewe, ingawa, na hiyo ndivyo tunatakiwa kufanya.

"Tuna mechi inayofuata nyumbani, dhidi ya Porto, na tunaweza kuifungia huko. Tunapaswa kurudisha hali ya kujiamini. Tunacheza kidogo hivi sasa.

# Kiwango cha Leao chamfurahisha Pioli

**PARIS,** Ufaransa

STEFANO Pioli alitoa sifa maalum kwa Rafael Leao baada ya winga huyo kuhamasisha ushindi muhimu wa AC Milan wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain, hapo juzi.

Leao alisawazisha bao la ufunguzi la Milan Skriniar kwa mkwaju mzuri wa juu dakika ya 12 kabla ya mpira wa kichwa wa kipindi cha pili wa Olivier Giroud kuipatia timu hiyo ya Italia ushindi wa 2-1.

Na baada ya kuanza kwa msimu kwa utulivu, bosi wa Milan alifurahi kumwona supastaa wake akija kwenye karamu ya Ligi ya Mabingwa.

Pioli alisema: "Hiki lazima kiwe kiwango chake.

"Anaweza kuwa bingwa. Alicheza mechi ya kipekee kama kila mtu mwingine, sio tu kwa ubora, lakini pia kwa suala la hamasa."

Ushindi wa mabingwa hao mara saba wa Ulaya pamoja na ushindi wa 2-0 wa Borussia Dortmund dhidi ya Newcastle Uniyed - umelipua Kundi F, huku timu zote nne zikiwa na uwezo wa kutinga hatua ya mtoano.

Na Pioli anajua baada ya mwendo mgumu wa kufanya vizuri, kikosi chake kitacheza na Dortmund katika raundi inayofuata ya mechi.

Alisema: "Tulichukua hatua muhimu mbele lakini kundi litaamuliwa tu katika raundi ya mwisho.

"Sasa tuna pambano la moja kwa moja na Dortmund ambao wako pointi mbili mbele yetu na inaweza kuwa ya maamuzi.

"Hongera kwa vijana. Ilikuwa mechi muhimu kwa kundi lakini hakuna kilichoamuliwa."

Baada ya kupokea kichapo kutoka kwa Udinese kwenye Serie A Jumamosi, Milan itazingatia kwanza kurejea katika hali ya nyumbani huko Lecce wikendi hii.

# YANGA YAPANGA KUSHUSHA 'MASHINE' MPYA DESEMBA

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanatimiza malengo yako kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa, uongozi wa Yanga umesema utaboresha kikosi chao wakati wa dirisha dogo la usajili kulingana na mapendekezo yatakayotolewa na benchi la ufundi, imefahamika.

**Dirisha dogo la usajili litafunguliwa kuanzia Desemba 16, mwaka huu na litafungwa ifikapo Januari 15, mwakani.**

Moja ya idara inayohitaji kuongezwa nguvu ni ya washambuliaji na hilo limetokana na maelekezo ya kocha, Miguel Gamondi kuhitaji makali zaidi katika safu hiyo.

Kwa sasa safu ya ushambuliaji ya Yanga inaongozwa na Clement Mzize, Kennedy Musonda na Hafiz Konkoni aliyesajiliwa dirisha kubwa ili kuziba nafasi ya Fiston Mayele, kitu ambacho hajaweza kuonyesha makali kama ilivyotarajiwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema watafanya usajili katika nafasi chache na tayari benchi la ufundi limeshaanza mchakato wa wachezaji wanaowahitaji.

Hersi alisema licha ya kuwapo na kikosi imara lakini bado wanahitaji kuboresha timu kwa sababu wanataka kufanya vizuri zaidi kuliko msimu uliopita.

"Tuna mashindano mengi na muda hautakuwa rafiki lakini tunatarajia kupokea mapendekezo kutoka kwa kocha juu ya nafasi gani anazotaka tufanye usajili. Mapendekezo yakitufikia, tutaenda kuyafanyia kazi haraka kwa sababu tuna mechi kubwa ikiwamo michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lazima tuongeze nguvu," alisema Hersi.

Kuhusu mbio za ubingwa, Hersi alisema ni mapema sana na kushinda mechi dhidi ya Simba haina maana njia ya kutwaa taji hilo ipo karibu.

"Ndio kwanza tumecheza michezo saba na wengine mitano, huwezi kudai ubingwa upo karibu, bado ligi inaendelea baada ya mechi yetu na Coastal Union kwa mwezi Novemba hatuna mechi nyingine hadi Februari ambapo ligi itaendelea.

Hapa kati tutapisha michuano ya AFCON, lakini Desemba tutakuwa na michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Januari tutaenda Mapinduzi, baada ya hapo ligi itaendelea na tutakuwa na mechi mfululizo," alisema rais huyo wa Yanga.

## Ahmed afunguka kutemwa Simba

**Na Mwandishi Wetu**

MENEJA wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema hana taarifa yoyote kutoka kwa mabosi wa klabu hiyo kuhusiana na yeye 'kukalia kuti kavu' katika nafasi yake anayoitumikia.

Baada ya Simba kupoteza mechi dhidi ya Yanga, kulikuwa na tetesi za ofisa huyo kusimamishwa pamoja na wachezaji watano huku tayari Kocha Mkuu, Roberto Oliviera 'Robertinho' amefukuzwa kazi.

Ahmed alisema yeye anaendelea vyema na majukumu yake lakini kama viongozi wake wataona kuna haja ya kufanya maboresho katika nafasi yake kwa manufaa ya Simba yupo tayari.

"Sina taarifa kutaka kuondolewa kwenye nafasi yangu, naendelea na majukumu yangu kama kawaida, lakini kama uongozi utakuwa na jambo lolote nitapewa taarifa na nitakubaliana na kile nitakachoelezwa," alisema Ahmed.

Aliongeza mechi dhidi ya Yanga imeshapita na sasa wanaelekeza akili na nguvu katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo utakaochezwa leo na kikubwa wamejipanga kusahihisha makosa ili kurejesha morali ya wachezaji wao.

## Mashabiki Tabora United wahuzunika

**Na Adam Fungamwango**

BAADHI ya mashabiki wa Tabora United ya mkoani Tabora inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara wameonyesha kutoridhishwa na matokeo ya timu yao, imefahamika.

Akizungumza baada ya mechi dhidi ya Geita Gold iliyochezwa Jumatatu iliyopita kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari, Nyankumbu, Geita na kumalizika kwa suluhu, Juma Salum, alisema haelewi ni kwa nini timu yao inashindwa kupata ushindi.

"Sisi kama mashabiki wa Tabora United ni lazima tuulize uongozi shida iko wapi, ni wachezaji au ni mwalimu, na kama tatizo ni la viongozi tujue nani wanasababisha hadi wachezaji wanakosa morali ya kupambana," Juma alisema.

Naye Haruna Msoga, alisema kutoka sare hasa ugenini si mbaya, lakini wanawataka viongozi wao kuongeza nguvu katika kipindi cha dirisha dogo ili kuhakikisha mzunguko wa pili wanakuwa imara na kufanya vyema.

"Hiki ndicho sijakielewa, kama tunatoka sare nje, basi tukija nyumbani tuwe tunashinda, wapinzani wanapataje sare hapa, lazima tukae chini na kufahamu wapi kuna tatizo, hatutaki kusubiri mambo yaharibike zaidi?" Alihoji Abdulrahman Slim.




Kiungo mkabaji wa Azam FC, Sospeter Bajana (kushoto), akishangilia bao pamoja na Yahya Zaid katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ihefu iliyochezwa kwenye Uwanja wa Highland Estates Mbarali, Mbeya wiki iliyopita. Azam ilishinda 3-1. **PICHA: MTANDAO**

## *Bajana afurahia rekodi Azam FC*

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkabaji wa Azam FC, Sospeter Bajana, amesema hatasahau rekodi ya kufunga mabao mawili katika mechi moja ambayo iliiweka Novemba 4, mwaka huu wakati timu yake ilipopata ushindi wa magoli 3-1 katika mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya wenyeji Ihefu.

Bajana alisema hajawahi kufunga mabao mawili katika mechi moja tangu aanze kucheza soka, hivyo kwake ni jambo la kukumbukwa daima.

Kiungo huyo alisema rekodi hiyo atatembea nayo katika maisha yake ya soka, hasa ikizingatiwa yeye anacheza eneo la kiungo mkabaji, hivyo amekuwa hafungi sana mabao na hata ikitokea anafunga goli moja tu.

"Yaani nashukuru Mungu, unajua hii ni mara yangu ya kwanza katika maisha yangu, nilikuwa sijawahi kufunga mabao mawili kwenye mechi moja tangu nianze kucheza soka, siku ya Novemba 4, mwaka huu nitaiweka katika kumbukumbu yangu ya soka hadi nastaafu, ni rekodi bora sana kwangu hasa ikizingatiwa kiungo wakabaji jukumu lao la kwanza si kufunga mabao," alisema Bajana.

Kuhusu mwenendo wa timu yake, alisema kwa sasa imerejea katika 'reli' baada ya kushinda mechi mbili mfululizo tena ikiwa ugenini.

"Kusema kweli tumerudi katika morali, tulipoteza mechi mbili mfululizo, tukakaa wenyewe kama wachezaji na kujiambia tuvute soksi tupambane, ndiyo tukaanza sasa kupata ushindi katika mechi mbili mfululizo," alisema mchezaji huyo.

# Michezo

Alhamisi Novemba 9, 2023

Nipashe





Casemiro kurudi dimbani Krismasi UKURASA 21




Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (katikati), akiruka na kufunga kwa kichwa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga jana. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga yaendeleza kicheko

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI waliotokea benchi, Clement Mzize na Jesus Moloko waliongoza Yanga kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga jana.

Kwa matokeo hayo, Yanga imeendelea kujiimarisha kileleni baada ya kufikisha pointi 24 huku Coastal Union ikisalia katika nafasi ya 13 na pointi zake saba, kila timu ikicheza mechi tisa.

Alikuwa ni Mzize aliyewainua mashabiki wa Yanga kwa kufunga bao pekee katika mechi hiyo dakika ya 70, aliporuka juu na kuunganishwa kwa kichwa mpira uliopigwa na Moloko ambaye wote waliingia kipindi cha pili.

Bao hilo lilikuwa linasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa timu hiyo katika mechi hiyo iliyokuwa kali na yenye ushindani ikiwa zimepita siku chache tangu wapate ushindi wa kishindo wa mabao 5-1 dhidi ya watazi wa jadi, Simba.

Mzize alitumia makosa ya kipa wa Coastal Union, Ley Matampi, ambaye alianza kutoka langoni kuifuata krosi hiyo, lakini baadaye akaghairi na wakati amesita kutaka kurudi ndiyo muda huo huo mfungaji akaifungia timu yake goli hilo.

Linakuwa ni bao la tatu ya Yanga kufungwa kwa kichwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kati ya mabao 26 waliyofunga msimu huu.

Sekunde wa 40 tu tayari Yanga ilikuwa imeshapiga hodi katika lango la Coastal Union kupitia kwa Maxi Nzengeli, alipounganisha krosi kutoka wingi ya kushoto iliyomiminwa na Nickson Kibabage, lakini shuti lake lilipaa juu ya lango.

Nzengeli aliambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto dakika ya 10, lakini shuti lake lilienda pembeni ya lango.

Coastal Union ilifanya mashambulizi mawili ya nguvu dakika ya 22, wakati Charles Semfuko alipowekea pasi safi na Miraji Hassan, lakini shuti lake lilipaa juu, na sekunde chache baadaye wakati Yanga wakianza vibaya mpira nyuma, Ibrahim Ajibu alimwekea straika, Enock Mayala akiwa kwenye eneo zuri la kuukwamisha mpira wavuni, lakini Mkongomani huyo alipiga nje.

Alikuwa ni Pacome Zouzoa ambaye aliingia kwenye orodha ya wachezaji waliokosa mabao, baada ya gonga za hapa na pale na wachezaji wenzake, alipiga shuti ambalo halikulenga lango.

Coastal ambayo kipindi cha kwanza ilionekana kukabia juu, ilibadilika kipindi cha pili na kurudi nyuma zaidi hali iliyofanya Yanga kutawala zaidi hadi kupata bao.

# Waziri: Simba nendeni TAKUKURU

**Na Waandishi Wetu**

●●● Kama imebaini 'harufu' ya rushwa katika dabi, kuivaa Namungo...

WAKATI Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, akiwataka Simba kutoa taarifa katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), endapo imebaini kuna viashiria vya rushwa katika mechi dhidi ya Yanga, Mnyama anakutana na Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

**Simba ilipokea kichapo cha bila huruma cha mabao 5-1 kutoka kwa Yanga katika mechi hiyo ya mzunguko wa kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili iliyopita.**

Hata hivyo hadi jana jioni, hakuna mchezaji yoyote wa Simba ambaye amesimamishwa kutokana na kichapo hicho, na nyota waliyokuwa wakitaja wanaendelea na mazoezi kama kawaida kwa ajili ya kuivaa Namungo.

Simbachawene alitoa agizo hilo jana bungeni jijini, Dodoma wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Makete, Festo Sanga, aliyetaka kujua kauli ya serikali kuhusu Simba kuwasimamisha baadhi ya wachezaji wake kwa madai ya kuwapo kwa viashiria vya rushwa katika mchezo huo.

Akiuliza swali hilo, Sanga alisema: "Kwa kuwa kumekua na viashiria vya rushwa michezoni ikiwamo mchezo uliopita wa Simba na Yanga, ambapo jana Bodi ya Klabu ya Simba imewasimamisha baadhi ya wachezaji wakihusishwa na vitendo hivyo, upi mkakati wa serikali wa kupambana na rushwa michezoni ili ligi yetu iwe safi."

Simbachawene akitolea ufafanuzi wa suala hilo, alisema vitendo vya rushwa michezoni havikubaliki, kama mchezo wa Jumapili wa Simba na Yanga unaviashiria vyovyote vya rushwa, Simba iende ikaripoti katika Ofisi ya TAKUKURU wilayani Temeke kama zile tano zimetokana na rushwa.

Awali akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA', alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), imekua ikipinga vitendo vya rushwa katika michezo na kwa kushirikiana na TAKUKURU wamekuwa wakitoa elimu kuhusu suala hilo.

Mwana FA alisema tayari wameanzisha kampeni inayoitwa 'Kataa upangaji wa matokeo, linda hadhi ya mpira wa miguu' ambayo inaendelea kuleta matokeo mazuri kwa kushirikiana na wadau wengine wa michezo vikiwamo vilabu husika kwa ajili ya kupinga vitendo hivyo.

Katika hatua nyingine, waziri huyo alisema serikali inaendelea kukarabati viwanja vya mpira wa miguu saba katika majiji ya Tanga, Morogoro, Dodoma na Arusha ili viwe na hadhi nzuri itakayokidhi kutumika katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kuelekea mechi ya leo, Kaimu Kocha Mkuu, Daniel Cadena, alisema wamefanyia kazi mapungufu mbalimbali yaliyojitokeza katika mechi iliyopita na sasa wamejipanga kutafuta pointi tatu muhimu ili kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi.

Cadena alisema kazi kubwa aliyoifanya ni kuandaa wachezaji kiakili, kimwili na kiufundi kuhakikisha wanapambana kupata matokeo mazuri katika mchezo huo kwa sababu bado nafasi ya kufikia malengo wanayo.

"Nawaheshimu wapinzani wetu, kila mechi imekuwa na maandalizi yake, wachezaji wako tayari kwa ajili ya kupambana kutafuta matokeo mazuri mechi ya kesho (leo)," alisema Cadena.

Nahodha wa Simba, John Bocco, alisema mechi hiyo haitakuwa mechi rahisi kwa sababu Namungo FC pia wanahitaji matokeo bora, hivyo wataingia kwa lengo la kupambana kusaka ushindi na tayari wamesahau matokeo ya mechi iliyopita.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo, Denis Kitambi, alisema wameona mapungufu ya Simba ambayo imeruhusu bao katika kila mchezo na hivyo maandalizi yao yalianzia hapo.

"Katika mechi zote nilizoiona kwa Simba ni jinsi wanapopata bao ndani ya dakika 5,10,15 na 20 wanapofunga wachezaji wanaridhika na kutocheza kwa presha ambayo walianza nayo. Al Ahly na Yanga wametupa mwanga wa kuona ubora na madhaifu ya Simba, katika maandalizi yangu sikuweza kuumiza kichwa sana jinsi gani ya kuingia katika mchezo huu," alisema Kitambi.

***Imeandaliwa na Saada Akida, DAR na Agusta Njoji, DODOMA.***


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >